**MWONGOZO MFUPI- Maelezo kwa ajili ya kuishi maisha ya umoja na ya kiroho**

*Ujumbe wa Papa Siku ya kutangazwa Mwenye Heri Kaka Karoli wa Foucauld;*
*Novemba 13, 2005 katika Basilika la Mtakatifu Petro, ROMA.*

Karoli wa Foucauld anatualika tufanye tafakari kuhusu fumbo la umwilisho; fumbo ambalo Nafsi ya Pili ya Mungu alifanyika mwanadamu.

Karoli alipata kuishi Nazareti ili aweze kumfahamu na kumfuasa vema Yesu Kristo. Alifanya hivyo kwa unyenyekevu na kwa kujikatalia mengi.

Kukaa kwake Nazareti kulimwezesha Karoli kufahamu kwamba Yesu Kristo kwa kuja kushiriki ubinadamu wetu, alitoa mwito wa kuishi maisha ya kushirikiana yaani maisha ya kidugu.

Karoli ambaye alikuwa Padre, anatueleza kwamba Ekaristi na Injili, ambavyo ni pacha wa madhabahu ya mkate na neno, ndio msingi wa maisha ya kikristo.

**UJUMBE WA KADINALI JOSE SARAIVA MARTINS**

Mchango wa Karoli katika maisha ya kiroho unazidi kuonekana kwenye karne yetu ya 20 hasa mwanzoni mwa milenia hii ya tatu. Hiki ni kipindi ambapo tunatakiwa kabisa kuishi kulingana na Injili.

Maisha ya Injili yanatuhimiza kuwa wanyofu; yanatuhimiza kuitangaza Injili pasipo kujitangaza wenyewe, yanatuhimiza kumshuhudia Kristo kwa kukubali utajiri wa kiroho walionao wenzetu, yanatuhimiza kuupa upendo nafasi ya kwanza na yanatualika kuelewa kwamba upeo wa upendo unathibitika katika maisha ya pamoja.

Tunaambiwa kwamba Mwenye heri Karoli alipeperusha kwa bidii zote Injili na kupaza ujumbe kuwa *'tuko mali ya Kristo'*

**DIBAJI**

Mwongozo huu mfupi umetayarishwa na iliyokuwa timu ya kimataifa ya walei wa 'Kaka Karoli wa Foucauld'

Mwongozo umepitiwa mara kadha na timu ya kimataifa iliyopo sasa madarakani hasa nyakati za mikutano iliyofanyika Uhispania (2001), Ujerumani (2003) na Tanzania (2004) ambapo Timu iliweza kuhariri, kusahihisha na kufanya nyongeza ili mradi mwongozo huu ukubalike katika mabara yote.

Bila shaka mwongozo huu mfupi utawanufaisha wanajumuiya zote na hasa zilizo katika hatua za awali. Vile vile mwongozo utakuwa ni chombo muhimu kwa masista na mabruda katika matawi mbalimbali yaliyo sehemu ya *familia ya kiroho ya Kaka Karoli.* Wao kwa msaada wa mwongozo huu wataweza kuwajengea moyo na uwezo wanafamilia hizo ili waunde jumuiya zingine mpya!

Mwongozo unayo maagizo machache ambayo yapo nje ya mazoea yetu; yamekuwa machache ili kwamba tujisikie huru bila ya kuwa na wasiwasi na hivyo kuwa na wasaa zaidi wa kumpenda Mungu.

Shabaha ya kanuni hii ni kutuwezesha kufikia maisha ya pamoja ambayo ni ya kawaida pasipo kuzongwa na yale yanayoweza kutuzuia kuwa na moyo wa kumtafakari Mungu ili tuweze kuishi kiuadilifu kama vile Mtakatifu Yosef alivyofanya huko Nazareti.

**Ifahamike kwamba mwongozo huu mfupi si sheria hasa bali ni maelekezo ambayo yatazingatiwa kuendana na haja za mahali husika!**

Katika sura tatu za mwanzo (I – III) kuna habari juu ya maisha ya Kaka Karoli wa Foucauld aidha maelekezo kuhusu jumuiya ya walei na maisha yao ya kiroho.

Sura ya IV inajadili jukumu la walei na habari za kanisa kwa ujumla. Sura ya V inaeleza sifa za maisha ya umoja. Sura ya VI inatupa mwongozo wa kiroho na namna ya kuishi pamoja. Sura ya VII inatuelekeza kwenye sala muhimu kulingana na mapokeo ya Kaka Karoli na maelezo mintaarafu chimbuko lake. Sura ya VIII inahitimisha mwongozo huu na kuna anwani mbalimbali.

Matayarisho ya mwongozo huu yalikamilika katika sikukuu ya Epifania 2006. *Mamajusi* waliifuata nyota iliyowaongoza mpaka Beltlehemu na hivyo kumwona kichanga aliye Mtakatifu. Macho yetu na yafunguke, tuione nyota itakayotuongoza kwa "Bwana mweza wa yote" aliye kwetu mfano pekee!

# SURA YA KWANZA

# KAROLI WA FOUCAULD: MAISHA NA UJUMBE

## 1.1. KAROLI WA FOUCAULD: 1858 – 1916

| | |
|---|---|
| **KUZALIWA: 1858** | • Alizaliwa 15 Septemba 1858 Strasburg nchini Ufaransa na kubatizwa akiwa mchanga. Familia yake ilikuwa ya tabaka ya juu na matajiri yenye kaulimbiu iliyosema "kamwe usikubali kushindwa" |
| **UTOTO HADI UJANA: 1858 – 1876**<br><br>***"Mimi ambaye nilizungukwa na neema nyingi tangu mapema utotoni… mtoto wa mama wa kiume aliye kama mtakatifu… Novemba 1897.*** | • Karoli alibahatika kuwa na mdogo wake wa kike aliyeitwa Maria.<br>• Kwa bahati mbaya wazazi wake walifariki mmoja baada ya mwingine mwaka 1864 na kumwachia pigo kubwa kimaisha.<br>• Babu yao mzaa mama aliwachukua . Alikuwa mpole mno na dhaifu .Akawa muungwana kwao.<br>• Wajerumani waliwashinda wafaransa katika vita ya 1870. Familia mpya ya Karoli ilihamia na kukaa sehemu ya Nancy, Ufaransa ambako Karoli aliweza kupelekwa shuleni.<br>• Baadaye Karoli alienda kusoma katika shule ya majezuiti hapo Ufaransa na kuhitimu elimu ya sekondari. Akawa na hamu ya kujiunga na jeshi. Kulingana na maelezo yake aliacha imani kabisa akiwa na umri wa miaka 16 tu. |
| **JESHINI 1876 – 1881**<br><br>***"Nilitangatanga na kupotea mbali nawe. Imani yote ilikuwa imetoweka"\| (Mafungo. Novemba 1897)*** | • 1876: Alijiunga na chuo cha kijeshi cha Mtakatifu Sirili. Akawa amefukuzwa kabla hajamaliza hata mwaka kwa sababu za uzembe.<br>• 1878: Babu mzaa mama alifariki na kumwachia mali. Akazitapanya. Alijiunga tena na shule na alihitimu 1879 akiwa wa mwisho darasani.<br>• 1879: Alipata ajira jeshini, akawa anaishi maisha ya anasa akiwa na mwanamke mpenzi.<br>• 1880: Kikosi chake kilienda Aljeria, akaandamana nacho pamoja na yule mwanamke. Jeshi likamfukuza baada ya kugundua hakuwa mke wake. Aliondoka na kurudi Ufaransa, akawa anakaa Evian.<br>• 1881: Aliomba kurejeshwa kwenye kikosi chake Tunisia, Aljeria. Alipokubaliwa aliachana na yule kimada. Kwa muda wa miezi 8 tu akajidhihirisha kuwa mpiganaji na kiongozi shupavu. Wakuu wake na kikosi kizima wakamsifia. |
| **MISAFARA YA UVUMBUZI 1882 – 1886** | • 1882: Aliamua kuacha jeshi kwa ajili ya kujiandaa na safari yenye lengo la kufanya utafiti sehemu za Moroko. Akawa amejifunza kiarabu na kiebrania.<br>• 1883 – 1884 alizunguka Moroko kwa kificho akiambatana na mzee Myahudi aliyeitwa Mardochee. Akavutiwa sana na imani na maisha ya sala ya waislamu.<br>• 1884: Karoli alipokuwa Aljeria alitaka kufanya mipango ya kuoa lakini ikishindikana baada ya kufarakana na familia yake<br>• 1885: Alipata tuzo ya medali ya dhahabu kutoka shirika la kijiografia la Ufaransa kufuatia taarifa yake kuhusu safari ya kiutafiti aliyoifanya Moroko.<br>• 1885 – 1886: Alisafiri kwenye chemichemi za jangwani kusini mwa Aljeria na Tunisia.<br>• 1886: Alirejea Ufaransa na kuimarisha uhusiano na jamaa zake hasa binamu yake aliyeitwa Maria.<br>. Alichapisha kitabu kilichojulikana kama *"Ugunduzi wa Moroko"*<br>. Akaanza kuishi maisha ya utulivu yenye kuzingatia maadili mema.<br>. Akajihoji katika maisha yake ya kiroho kwa undani zaidi.<br>. Japo imani yake bado ilikuwa haba, aliweza kujenga mazoea ya kwenda kanisani na akasali sala hii mara nyingi *"Mungu, kama upo basi jifunue kwangu"* |

| | |
|---|---|
| **UONGOFU**<br>**1886 – 1889**<br><br>***"Mara nilipoamini kwamba Mungu yupo, nilikata shauri ya kuishi kwa ajili yake tu na si vinginevyo"***<br>***14 Agosti 1901.*** | • Mwishoni mwa Oktoba 1886: Alienda kumwomba Padre Huvelin ushauri wa kiroho. Binamu yake Maria alimwelekeza kwa padre huyo ambaye alikuwa katika kanisa la Mtakatifu Agustino- Ufaransa, Paris.<br>• Padre alimpatia kitubio mara moja na akampa komunyo.<br>• 1887 – 1888 alianza kutamani kuwa mtawa.<br>• 1888 – 1889: Karoli alizuru Nchi Takatifu ambako alipata mwamko wa kipekee kiimani.<br>• Aliporejea Ufaransa alikabidhi vitu vyake vyote kwa Maria, akaanza kufunga kwa lengo la kubaini utawa atakaoweza kujiunga nao.<br>• Akajisikia kwenda kuishi maisha ya upweke, ufukara na unyoofu kwa namna ya mtumishi huko Nazareti.<br>• Akawa amependelea kwenda kuishi maisha ya utawa wa kimonaki wa ndani. |
| **MAISHA YA KITAWA**<br>**1890 – 1897**<br><br>***"Mwito wangu wa kuishi kitawa pamoja na imani yangu vilichipuka vyote kwa wakati moja".***<br>Barua: 14/08/1901. | • 15/01/1890: Alijiunga na monasteri ya wakaa pweke/kimya iliyojulikana 'Bibi Yetu wa Theluji' ambayo ilikuwa Ufaransa, Hata hivyo alikuwa bado na hamu zaidi ya kujiunga na monasteri ambako walikuwepo wakaa pweke fukara zaidi huko Akbes, Siria. Alifanikiwa kwenda huko miezi 6 baadaye.<br>• Aliandaa kanuni ya maisha ya kitawa na kuipa jina la 'Naitamani Nazareti'<br>• 1896 baada ya kuomba kuahirishiwa nadhiri zake, alipelekwa masomoni Roma.<br>• Januari 1897: Abati Mkuu wa wamonaki wakaa pweke aliridhia utashi wa Karoli na kumruhusu kuchagua mwito atakaouchagua. |
| **NAZARETI**<br>**1897 – 1900**<br><br>***"Walau nifanane na Kristo…"***<br>Barua 14/08/1901<br><br>***"Kwa kuadhimisha Misa, kutanifanya nimlipe Mungu zawadi iliyo kuu, kuwatendea wema wanadamu"***<br>Barua: 26/04/1900 | • Machi 1897: Alienda kuishi Nazareti na akawa mfanyakazi wa kutwa kwenye nyumba ya watawa, masista wa Mtakatifu Klara. Kibanda chake cha kuishi kilikuwa pembezoni mwa nyumba ya watawa hao.<br>• "Nilipata ruhusa kwenda kuishi Nazareti nikiwa peke yangu, tena sikujulikana zaidi ya kufahamika kama mfanyakazi wa kutwa nikifanya kazi za kila siku, nikiwa pekee, nikizingatia sala, kuabudu, tafakari ya Injili, na kazi ya kujinyenyekesha"<br>• Alikaa Nazareti kwa miaka 3. Baadaye watawa wa Mtakatifu Klara na aliyekuwa mwungamishi wao Padre Huvelin wakamshauri aombe kupewa daraja Takatifu ya Upadre.<br>• Alirejea Ufaransa kwenye monasteri mojawapo ambako alifanya matayarisho ya kupokea daraja takatifu.<br>• Juni 9, 1901: Alipewa Daraja Takatifu ya Upadre Viviers, Ufaransa |
| **NCHINI ALJERIA**<br>**1901 – 1906**<br><br>"***Naenda kuishi jangwani maisha ya kutoonekana hadharani kama ya Yesu wa Nazareti, si kwa nia ya kuhubiri, bali kuishi kwa faragha, ufukara na unyenyekevu kama Yesu"***<br>Aprili 1904 | • Septemba 1901: Karoli alirejea Aljeria na kukaa mahali paitwapo Beni-Abbes na kujenga makao ya watawa wakaa pweke. Aliona aanzishe umoja wa watawa wa ndani utakaojulikana kama 'Kaka wadogo wa Moyo Mtakatifu wa Yesu'.<br>• 1902: Aliwatahadharisha marafiki na mamlaka husika juu ya madhila ya utumwa.<br>• Aliwaweka huru baadhi ya watumwa baada ya kulipa malipo ya kuwakomboa.<br>• 1904 – 1905: Alisafiri mara kadhaa kwenda kwa Watuareg katika jangwa la Sahara ambako alijifunza lugha za wenyeji wa huko. Alikuwa padre wa kwanza kufika huko.Mwaka 1905, alihamia Tamanrasset.<br>• Alianza kutafsiri Injili kwenda katika lugha ya ki Tuareg.<br>• 1906: Alimpata mwenzi aliyeitwa Bruda Mikael lakini aliugua ghafla na kurejea Ufaransa. |
| **SAFARI ZA MARA KWA MARA UFARANSA**<br>1907 – 1916 | • Julai 1907: Karoli alikabiliana na kazi nyingine nzito ya kitaalam, nayo ni kutafsiri nyimbo na mashairi ya Watuareg Aliweza kufanya hivyo kwa msaada wa wenyeji.<br>• Alizuiliwa kuadhimisha Ekaristi Takatifu kwa vile alikuwa ndiye mkristo pekee. Baada ya miezi 6 aliweza kupata ruhusa kuadhimisha misa takatifu |

| | |
|---|---|
| ***"Utume wangu sherti uwe ni utume wa kutenda mema. Kutoka kwangu watu wataweza kuelezana kuwa kwa vile huyu amekuwa mwema kiasi hiki, bila shaka dini yake pia itakuwa nzuri"*** <br>1909. | peke yake bila uwezo wa kuhifadhi hostia takatifu.<br>• Januari 1908: Alikabiliwa na dhiki iliyotokana na njaa kuu wakati ule, akaugua na akadhoofu mno nusura afe! Wenyeji walimhifadhi kwa kumgawia maziwa ya mbuzi. Hakika alionja upendo na umuhimu wa ujirani mwema hasa katika dhana ya kupokea na kutoa.<br>• 1909 – 1911 -1913: Alizuru Ufaransa mara tatu kwa lengo la kujadiliana na wakuu wa shirika juu ya uwezekano wa kuwepo "Umoja wa mabruda na masista wa Moyo Mtakatifu wa Yesu" ambao utashughulika na uongofu wa wasioamini. "Wakristo wenye bidii, bila kujali aina ya maisha waliyonayo, watambuliwe kama wakristo wenye imani kutokana na jinsi wanavyoweza kuishi Injili kwa vitendo. *(Sheria na Mashauri, 1910 – 1913)*<br>• 1914: Vita vya kwanza vya dunia viliibuka Ulaya. Karoli alibaki Tamanrasset baada ya kushauriwa na jenerali Laperrine ambaye alikuwa rafiki yake.<br>• 1915: Uvamizi wa mara kwa mara uliofanywa na wamoroko na wa senoussites waliotoka Libya ulileta hali ya kukosekana utulivu na amani. |
| **KIFO CHAKE**<br>1916<br>"Punje ya ngano hubaki punje tu isipokuwa ikianguka katika udongo na kufa. kama ikifa huzaa matunda mengi."<br><br>Jn:12,24 | • Alijenga ngome ndogo Tamanrasset kuwasalimisha wakazi wa hapo. Aliweza kuishi humo kwa lengo la kuwapokea watakao kuwa wakimbizi.<br>• Aliendelea na kutafsiri mashairi na mithali za Watuareg.<br>• Desemba 1, 1916: Wa tuareg walimhadaa akatoka nje ya ngome kisha wakamkamata na kumfunga.<br>• Uporaji na utekaji nyara uliofanywa na wanajeshi wa kifaransa ulileta wasiwasi miongoni mwa raia kwani hawakujua ni lini wanaweza kuvamiwa. Katika pilika ya uporaji mlipuko wa risasi ukamwua Karoli. Alizikwa kwenye handaki lililokuwa karibu na ngome.<br>• Kifo kilimkuta Karoli akiwa pekee ingawaje muda huo tayari kulikuwepo wanaumoja wa mabruda na masista wa Moyo Mtakatifu wapatao 49 nchini Ufaransa. Wanaumoja walikuwa wameshafanikiwa kupata kibali kutoka kwa wakuu kuanzisha huo umoja.<br>• Alitangazwa mwenye heri Novemba 13 mjini Roma.<br>• Leo hii kuna makundi tofauti 19 ya walei, mapadre, watawa wa kiume na wa kike, wanaoishi Injili ulimwenguni kote wakizingatia mang'amuzi na karama za Karoli wa Foucauld. |

### 1.2. Karoli wa Foucauld, Mtu katika enzi zake na Nabii wa leo

Kuna tofauti kubwa baina ya hatima ya Karoli na historia yake ya mwanzo; ukivilinganisha hivi viwili yaani mwanzo na mwisho wa maisha yake, utaona kwamba hakuwa mtu wa kawaida bali alikuwa ni mtu wa pekee. Karoli kama mtu tu haiba yake haiendani na uzito wa ujumbe wake wa kiroho ambao leo hii umekuwa ni mwongozo kwa wafuasi wake wengi duniani.

### 1. Karoli wa Foucauld: katika enzi zake.

Ukibaki na picha ya yule Karoli aliyekuwa mtoto katika familia ya yabaka ya juu na matajiri, ama Karoli aliyebobea katika anasa, kadhalika katika maisha yake jeshini, kisha ukamtazama wakati ule hisia zake zikiwa zimetibuka na visasi vya uonevu vilivyofanywa na majeshi ya wavamizi, uchungu uliotokana na vifo vya wazazi wake n.k. kisha kumtazama tena akisafiri huku na huko hadi Moroko na Aljeria, ambako utafiti wake umetoa mchango muhimu katika kufahamika utamaduni wa Watuareg; utabaini mengi!

**II. Ujumbe wa Karoli wa Foucauld: "Hebu tuirejee Injili"**

Karoli alifuata mifano ya watakatifu wakubwa kama vile Francis wa Assisi ambao Mungu aliwatukuza kutokana na bidii yao ya kuwahubiria wakristo ili wauishi vema ujumbe wa Injili. Karoli anasema "Tuirejee Injili, la sivyo Kristo hataishi miongoni mwetu" Kuirejea Injili ni kumkubali Yesu wa Nazareti kufanya makao mwetu kwa kuishi maisha ya umaskini wa roho, kujitoa kwa wote huku tukijiweka katika daraja ya chini, kujitolea kwa ajili ya wenzetu, n.k.

Kaka Karoli, akijawa na mapendo ya dhati kwa Yesu, alijitoa kikamilifu kuishi Injili. Ni kutokana na msingi huu, sisi tulio wanafamilia ya Karoli pamoja na wengi wa wale wanaojumuika nasi, sote tumeweza kuchota nguvu na mwanga.

**III. Karoli wa Foucauld, Nabii wa leo**

Kurejea kwenye Injili ni jambo la msingi kwa maisha ya kikristo, kadhalika kuna mambo ambayo nayo ni muhimu sana katika dunia yetu ya leo.

i. Karoli wa Foucauld alikuwa na kiu ya kiroho

- Ujana wake aliuishi kwa kukosa imani. Yeye ni mfano dhahiri kwa vijana wanaotafuta mwelekeo wa maisha.
- Maisha yake yote yalikuwa ni ya mahangaiko kwa ajili ya Yesu wa Nazareti. Aliweza kutambua mapenzi ya Mungu kupitia matukio mbalimbali. Katika ulimwengu huu wenye kubadilika kwa kasi, Karoli anaweza kutusaidia katika kukabiliana na mabadiliko haya ili kukidhi mahitaji yetu ya kiimani.

ii. Nazareti: Ni jambo la maana kujaribu kuoanisha swala la kujitoa kwa Mungu na vile vile kujitoa kwa watu wote; waume kwa wake. Katika kujitoa kwa Mungu, Karoli aliamua kuwa mmonaki, hata hivyo hakujitenga kabisa na watu, badala yake aliendelea kuwa karibu nao. Alipokuwa Tamanrasset aliendelea kuwa mtu wa kawaida miongoni mwao hao. Alikuwa rafiki tu wa kawaida lakini akashikamana nao kwa namna ya pekee hasa kwa walioonewa na kunyanyaswa, mathalani, juhudi zake za kupinga biashara ya utumwa.

Alijichanganya vema na Watuareg japo akionekana kuwaheshimu vilivyo, akajiahidi kuwaelewa kwa njia ya utafiti wake wa kitaalam kwa lengo la kuufanya utamaduni wao upendeke na kujulikana kwa mataifa,

iii. Katika kuwajali walio mbali: Alikubali kuwashirikisha wengine imani yake kwa Yesu Kristo kwa njia ya wito wa upadre. Akiwa padre alijitoa kikamilifu kwa ajili ya tabaka lililodharauliwa, kwanza kabisa kwa watu wa Moroko, lakini baada ya kushindwa kufika huko aliwaendea watu wanaokaa katika chemchemi za jangwani, na kuwa mwenyeji wa Watuareg. Miaka yake yote kuelekea ukingoni mwa maisha yake aliitumia kuwatangazia habari njema wenyeji hao.

iv. Kuwajengea wanyonge maisha ya kidugu popote pasipo kujali mipaka ya nchi, utaifa, ukabila, rangi na kuwafanya wanyonge wawe kiini cha jamii na cha kanisa.

v. Kanisa liwezeshwe kuishi kama Taifa la Mungu: Si tu kama mfumo wa utawala ambako kuna mabwana na watwana, ila kanisa kama wana wa Mungu, ambamo baadhi yao wanakuwa na utumishi wa kutoa huduma.

"Karoli wa Foucauld tangu awali aliamini kuwa wote wameitwa kwa njia ya ubatizo! Katika shirika lake alilolikusudia kulianzisha hakutarajia iwepo namna tofauti itakayoleta mgawanyo kati ya mapadre, mabruda na masista. Shirika lingewapokea wote; walei, watawa na mapadre.

Kwa namna hiyo alitarajia kuwaalika walei kushiriki katika utume wake jinsi ambavyo Mtakatifu Paulo alivyowashirikisha Prisila na Akwila katika kanisa la mwanzo. (Mdo. 18: 1-4; 18: 19-20".

***Maswali.***

1. ***Je nimeweza kubaini nini kutokana na tafakari yangu juu ya maisha ya Karoli wa Foucauld?***
2. ***Ni nini hasa ambacho naweza kuiga ambacho kinaendana kabisa na maisha yangu, uhusiano wangu na Mungu na wa watu wengine?***
3. ***Ni kwa namna gani maisha na ujumbe wa Kaka Karoli utanisaidia vilivyo kumfuasa Kristo?***
4. ***Napata ujumbe gani? Huo ujumbe nitauishi vipi katika maisha yangu ya kila siku?***

# SURA YA PILI

# FAMILIA YA KIROHO YA KAROLI WA FOUCAULD

## 3.1. Familia ya kiroho ya Karoli wa Foucauld

***"Endapo punje ya ngano haitadondoka ardhini na kufa, haitazaa, lakini ikifa, huzaa sana matunda" Yn. 12: 24.***

Leo hii yapo mashirika kumi ya kitawa na tisa ya wanachama wa maisha ya kiroho ambayo huunda Familia ya Kiroho ya Kaka Karoli

- Sodality Union- Umoja wa Ushirikano.
- Kundi la Karoli wa Foucauld (GCF)
- Dada Wadogo wa Moyo Mtakatifu (LSSH)
- Kaka Wadogo wa Yesu (LBJ)
- Dada wadogo wa Yesu (LSJ)
- Umoja wa mapadre wa Upendo wa Yesu (PrFrJC)
- Umoja wa Upendo wa Yesu (JCF)
- Umoja wa walei wa Karoli wa Foucauld (LayFr)
- Kaka wadogo wa Injili (LBG)
- Dada wadogo wa Injili (LSG)
- Dada wadogo wa Nazareti (LSN)
- Jumuiya ya Yesu (CJ)
- Kaka wadogo wa Upendo wa Yesu (LBJC)
- Kaka wadogo wa Umwilisho (LBI)
- Dada wadogo wa Moyo wa Yesu (LSHJ)
- Kaka wadogo wa Msalaba (LBC)
- Dada wadogo wa Umwilisho (LSI)
- Umoja wa Karoli wa Foucauld (FCF)
- Wamisionari wa Yesu Mtumishi (TSGTT)

### 3.2. Familia kubwa

Karoli wa Foucauld alipofariki Desemba Mosi 1916, tayari kulikuwa na orodha ya majina ya watu 49, likiwemo jina lake, wakiwa ni wanachama wa *"Umoja wa Kaka na Dada wa Moyo Mtakatifu wa Yesu"*, umoja ambao katika siku za mwisho wa uhai wake alijitahidi kuunda na kuandika mwongozo juu yake. Katibu wa umoja huo, Padre Laurian aliandika hivi "Kifo chake kimesambaratisha kila kitu" na hivyo ndivyo walivyofikiri wengi kwamba kikundi sasa kilikuwa kinatoweka!

Mtu pekee ambaye hakukata tamaa alikuwa ni Louis Massignon (1882 – 1962). Kwa mara ya kwanza alikutana na Karoli mnamo 1909, kisha akawa anawasiliana naye hadi alipofariki. Louis alifanya kila lililowezekana kuudumisha umoja huo. Aliweza kuuchapisha mwongozo ambao Karoli alikwisha uandaa kwa ajili ya Umoja. Louis mwenyewe naye alianzisha *Umoja wa Karoli wa Foucauld* baada ya kupata kibali cha Kardinali Amette. Aliandika Kitabu juu ya maisha ya Karoli na kukipa jina la *"Karoli wa Foucauld, Mgunduzi wa Moroko, Mtawa jangwani Sahara"*. Kitabu hiki kiliweza kumfanya Karoli afahamike hasa juu ya ujumbe wake, matokeo yake vikundi vya kiroho na mashirika ya kitawa yalianzishwa. Louis Massignon alitoa ushirikiano uliohitajika kwa vikundi na mashirika hayo.

Louis aliweza kuanzisha kikundi kingine kilichojulikana "Sodality Union" kilichowajumuisha waume kwa wake ambao ni walei, watawa, mabdruda, masista na mapadre. Umoja huu uliishi kulingana na Mwongozo aliouandika Karoli. Leo hii kikundi hiki kinajulikana kama "Sodality Union" na kimeenea katika mabara yote matano.

#### Vikundi vya mwanzo

Wito wa Kaka Karoli daima ulikuwa *"Tunawahitaji wakristo wa aina ya Prisilla na Akwila wenye kutenda mema bila makeke"*. Ujumbe huu ulimfanya Susana Garde aanze kutafakari namna ambavyo ujumbe wa Karoli ungeweza kudhihirika katika Afrika ya Kaskazini. "Akina mama wanapaswa kuinjilisha, wanaweza wakaanza kwa kuendesha huduma ya zahanati, ama kiwanda kidogo cha ushonaji, au kwa kufanya jambo lolote litakalowawezesha waarabu kuikubali imani". Huu ukawa ndio mwanzo wa Kikundi cha **Karoli wa Foucauld** nchini Aljeria, ambacho kiliweza kuenea baadaye sehemu za Tlemeen, El Bayad, na huko Dalidah karibu na mpaka wa Tunisia. Waaljeria walipoanzisha vita vya kupigania uhuru, kikundi kilihamisha makao yake hadi Ufaransa kwenye eneo la Bonne Encontre, jirani na Agen.

Katika kipindi hicho hicho kikundi cha **Wauguzi wa Bibi Yetu wa Carthage** kilianzishwa Tunisia kwa ushauri wa Askofu wa hapo ambaye 1924 aliridhia matumizi ya mwongozo wa Karoli wa Foucauld. Mnamo 1961 wauguzi hao akiwemo padre **Charles Henrion** na **Emile Malcor** walihamia Villecroze, Ufaransa ambako leo hii amebaki sista mmoja tu katika nyumba ya wazee na kikundi chenyewe hakipo tena.

Katika mwaka 1927 Padre Albert Peyriguere aliondoka alikokuwa akiishi Aljeria na alihamia Moroko eneo la El Kbab kwenye mkoa wa Kati hadi alipofariki 1959. Makazi yake yaliendelezwa na padre Michel Lafon ambaye alipenda kujulikana kwa jina la mmonaki-mmisionari, jina ambalo pia Karoli alipenda kujiita!

Miaka kadhaa baadaye walijitokeza watawa mbalimbali. Ilipofika Agosti 1933, **Umoja wa Dada Wadogo wa Moyo Mtakatifu** ulianzishwa na Sista Maria Karoli, jirani na Montpellier (Ufaransa). Mwezi moja baadaye Rene Voillaume na mabdruda wapatao wanne walipokea mwongozo kutoka **Kaka Wadogo wa Yesu** na kuanzisha kwa mara ya kwanza umoja ama

jumuiya yao nchini Aljeria. Mnamo 1939 Dada mdogo Magdalena na mwenzake waliweka ahadi za kuwa **Dada Wadogo wa Yesu**, wakakaa huko huko Aljeria sehemu za Touggourt miongoni kabisa mwa jamii zenye kuhama hama. Ingawaje vikundi hivi vitatu vilitofautiana katika baadhi ya mambo, lakini vilifanana katika kuishi maisha ya kufanya tafakari na ya umisionari.

**Kaka Wadogo wa Yesu** na **Dada Wadogo wa Moyo Mtakatifu** walianza kwa kuishi maisha ya umonaki. Lakini baada ya vita ya pili vya dunia na hasa baada ya Mtaguso wa Pili wa Vatikano walibadilisha mfumo huo wa maisha. Jumuiya ndogo ziliundwa zenye mwelekeo wa kuishi karibu kabisa na matabaka ya watu. Ujumbe uliotawala katika maisha haya ulikuwa 'Nazareti', kumtafuta Mungu kwa kufuata nyayo za Yesu ambaye aliishi maisha ya kawaida kila siku. Jumuiya za kidugu ziliundwa miongoni mwa matabaka ya walala hoi.

**Umoja wa wana Nazareti wa Karoli wa Foucauld** uliundwa 1947 kule Bordeaux, Ufaransa na Magdalena wa Vimont kwa ajili ya kuwahudumia wenye magonjwa ya akili. Kwa bahati mbaya umoja huu ulitoweka.

**Kitabu cha "Ndani mwa Mioyo ya watu" na Mabadiliko zaidi**

Padre Voillaume alichapisha kitabu kilichoitwa *"Au Coeur des masses" Seeds of the desert""Kati ya maisha ya watu"* ambacho kilieleza maisha ya **Kaka Wadogo wa Yesu**, jinsi ambavyo walimfuasa Kaka Karoli na namna walivyouelewa ujumbe wake.

Kitabu kilitoa mwaliko kwa kila mkristo kuishi maisha yenye uhusiano mwema na Mungu, na jinsi ya kuishi maisha yenye kujawa na tafakari inayogusa 'hadi kwenye mtima wa maisha ya sasa'.

Kitabu kilikuwa na ushawishi wa aina yake, kikawa kikitafsiriwa kwenda lugha mbalimbali. Ama kwa njia ya kitabu hiki wengi waliweza kumjua Karoli wa Foucauld pamoja na maisha yake ya kiroho.

**Umoja wa Walei wa Karoli wa Foucauld** ulitambuliwa rasmi na Askofu wa Jimbo la Aix-en, Mhashamu Provencheres, 1950. Kabla yake, vikundi vya wakristo katika miji mbalimbali nchini Ufaransa vilikuwa vikijumuika kwa lengo la kumfuasa Yesu Kristo na kujengeana uwezo wa kuishi Injili kulingana na mtazamo wa Kaka Karoli. Vikundi hivi viliwajumuisha wake kwa waume, waliooana na wasiooana, walei kwa mapadre. Leo hii Umoja wa Walei umeenea katika kila bara, ilhali vikundi vipya mara kwa mara. Hiki ndicho kikundi kikubwa kuliko vyote kutokana na idadi ya wanachama.

Mapadre ambao ni sehemu ya Umoja wa Walei walikuwa wakijumuika wao kwa wao kuona ni jinsi gani wanavyoweza wakajitoa kikamilifu wakiwa mapadre ili kuupatia utume wa kiinjili ladha ya Kaka Karoli. Ikawa umoja wa mapadre umeundwa na ukajulikana **Umoja wa Mapadre wa Upendo wa Yesu**, 1976. Kwa sasa umoja huu
umeenea katika mabara yote!

Katika kipindi hicho hicho, baadhi ya vijana wa kike ambao ni wakristo walihiari kuingia maisha ya kufanya tafakari kwa njia ya wao kuwa mabikira, kuweka ahadi, pasipokuacha kufanya kazi zao za kitaalam kwenye jamii, na pasipo kuingia maisha ya kitawa. Matokeo yakawa kuanzishwa kwa **Umoja wa Upendo wa Yesu** ambao mwanzilishi wake ni Marquerite Poncet mnamo 1952. Kikundi hiki kilitambuliwa kama taasisi rasmi ya wanawake na 1991 kiliweza kuzaa kikundi kingine ambacho kinaitwa **Umoja wa Karoli wa Foucauld** ambao ni umoja wa walei wanawake wenye lengo la kuishi useja yaani usafi wa moyo.

Kutokana na uzoefu alioupata kupitia **Kaka Wadogo wa Yesu**, Padre Voillaume alipata wazo la kuwa na jumuiya ambayo itaweza kufanya tafakari kuhusu neno la Mungu kwa kuhusianisha mahitaji ya walalahoi hasa kwa kushughulikia maendeleo yao ya kimwili na kiroho. Ndipo 1956 alianzisha **Kaka Wadogo wa Injili**, na baadaye 1963, **Dada Wadogo wa Injili.**

**Mkutano wa Beni-Abbes (1955) na Umoja wa Familia ya Kiroho ya Karoli wa Foucauld.**

Lengo la mkutano huo lilikuwa kuona jinsi ya kuviimarisha vikundi mbalimbali vilivyoundwa kutokana na kumfuasa Kaka Karoli. Tofauti katika aina ya miito ambayo ilibainika kwenye vikundi mbalimbali ilizingatiwa na kuthaminiwa. Aidha dhana ya kupingana na ukoloni mkongwe pia ilijitokeza huku wajumbe wengi wa mkutano wakiona haja ya kumtangaza Kaka Karoli kama Mtetezi wa 'ustaarabu wa kikristo' dhidi ya harakati za wapigania uhuru kutoka Afrika ya Kaskazini (Maghreb). Kulikuwepo na haja ya kuwa na 'umoja wa wakilishi' ambao ungejihusisha na kujibu au kutetea msemo uliokuwepo wa 'umoja ni popote', ili ubaki kuwa ni ujumbe wa kweli na usitumike kwa malengo ambayo hayakukusudiwa.

Mkutano uliishwa Beni-Abbes Novemba 14 hadi 16, 1955 chini ya uongozi wa Mhashamu Mercier, Askofu wa Sahara. Askofu Provencheres wa jimbo la Aix en Provence alishiriki pia na ndiye aliyekuwa akivipigania na kuvitetea vikundi mbalimbali vilivyoanzishwa. Wengine waliohudhuria ni pamoja na Askofu wa Montpellier, Mhashamu Duperray, Padre Peyriguere , wawakilishi wa vikundi mbalimbali vilivokuwa hai hasa waanzilishi wake pia walishiriki. Mkutano ama hija hio ilianzishwa na Neno la Mungu na sala. Na ndipo ukaanzishwa Umoja wa Padre Karoli wa Yesu. Shabaha ya umoja huo ilikuwa ni kudumisha umoja wa kiroho wa vikundi mbalimbali ambavyo vilianzishwa chini ya fikara na maisha ya kiroho ya Kaka Karoli. Kulikuwa na hiaji la kumfanya Karoli ajulikane vema kwa njia ya maisha (haiba) yake na kwa njia ya maandiko yake, na ikiwezekana kuhifadhi na kulinda kumbukumbu zake la sivyo zingepotea ama kupotoshwa. Pia iliamuliwa kuanzishwa kwa jarida la Yesu-Upendo ili liwe kiungo kati ya vikundi vyote kwa kushirikishana maisha ya kiroho.

Hivi sasa umoja huu unajulikana kama **Umoja wa Familia ya kiroho ya Karoli wa Foucauld**. Umoja unaendelea kupokea wanachama wapya hadi leo hii. Cha kushangaza ni kwamba wanachama wapya wanaendelea kupatikana nje kabisa ya Ufaransa, ingawaje ni huko huko Ulaya na katika mabara mengine.

**Familia ingali inakua**

Mnamo Agosti 15, 1966 **Dada wadogo wa Nazareti** walianza rasmi mjini Gent, Ubelgiji. Hawa ni vijana wa kike ambao ni wanachama wa Vijana Wakaoliki Wafanyakazi (VIWAWA). Dhamira yao ni kuishi ujumbe wa Kaka Karoli na wa Kardinali Cardjin wakilenga kuishi namna fulani ya maisha isiyojitofautisha na maisha ya kawaida ya watu wengine. Azma yao ni kuwahubiria wote wanaoishi nao kwamba 'maisha yao ni ya thamani kuliko dhahabu yote ipatikanayo duniani'

Mapema 1960 huko Katalonia Uhispania, utume miongoni mwa vijana ulipata msisimko baada ya muasisi wake Padre Vilaplana kupata mvuto wa kipekee kutokana na safari za kiroho za Kaka Karoli wa Foucauld kadiri zilivyoandikwa na Yohana Fransis na pia barua za Padre Peyriguere na kuamua kujihusisha na vijana. Padre Vilaplana akawa mvuto kwa vijana ambao walihiari kujitoa kwa ajili ya Bwana, ama kwa njia ya maisha yao ya ndoa ambako kila nyumba ilikuwa ni kama jumuiya, au kwa kuishi useja kwenye jumuiya ndogo. Ahadi za kwanza zilifanyika 1968 na **Jumuiya ya Yesu** ikaundwa.

Huko Jimbo la Foligno, Italia **jumuiya** iliyoanzishwa na Giancarlo Sibilia ya **Kaka wadogo wa Upendo wa Yesu** ilipata idhini kutoka kwa Askofu wa hilo jimbo. Jumuiya iliwajumuisha mapadre ambao walipenda kuishi maisha ya kimonaki, na hasa kufungamana katika maisha kidugu pasipo kuathiri huduma za kawaida za kichungaji walizokuwa wakizitoa jimboni.

Huko nchini Haiti, **Kaka na Dada wadogo wa Umwilisho** walianzisha umoja, waanzilishi wakiwa Franklin Armand kwa upande wa akina kaka (1976) na Emmanuela Victor kwa upande wa akina dada (1985). Ikumbukwe kuwa Haiti ni nchi ambayo imekuwa ikikumbwa na majanga mbalimbali! Wana umwilisho waliamani kuwa wakiwa kama wakulima kwa ajili ya wakulima, wataweza kumuishi Kristo na kuishi Injili na hivyo kutoa huduma katika kazi za maendeleo na uinjilishaji hasa vijijini.

Jimboni Bangui katika Afrika ya Kati, jumuiya ya watawa wa kike ilianzishwa 1977: Dada **Wadogo wa Moyo Makatifu wa Yesu**. Nchi ya Afrika ya Kati ina misukosuko ya kisiasa na ni maskini sana, lakini umoja iliopo kutokana na sala, ukarimu kwa kila anayejitokeza, na kujitoa kwa ajili ya huduma ya wengine, kumeifanya Afrika ya Kati pawe mahali pa amani!

Mwaka 1980, nchini Kanada, jumuiya ya kimonaki ya **Kaka Wadogo wa Msalaba** ilianzishwa chini ya Padre Mikael Verret (Kaka Mikael Maria wa Msalaba). Kwa kumfuasa Kaka Karoli waliamua kuishi kama jumuiya ya upendo ya wamonaki wakiwa tayari kumkaribisha yeyote atakayebisha hodi kwao.

Kikundi kilichoundwa miaka ya karibuni (1980) kipo nchini Vietnam nacho kinajulikana kama **Taasisi isiyokuwa ya kitawa ya Wamisionari wa Yesu Mtumishi** ambayo kifupi **chake ni TSGTT**. Kikundi kinajumuisha matawi ya vikundi vya wanaume, tawi moja la wanawake na tawi moja la wanachama washiriki. Ama kweli hili ni kundi kubwa na ambalo bado linazidi kuwashirikisha hata wasio wanachama.

**Jumuiya za K.Karoli** inawavuta wengi kwa vile haiba ya Kaka Karoli imewavuvia hamu ya kuipenda Injili na kuwapenda watu. Hamu hii imegusa mioyo yao kwa kina na kuwaachia kiu ya mambo ya kiroho.

**"Association":Umoja wa Familia ya kiroho ya kaka Karoli** hufanya mkutano mkuu kila baada ya miaka miwili. Hiyo ni fursa kwa viongozi wa vikundi mbalimbali kujumuika na kubadilishana uzoefu. Timu huchaguliwa wakati wa mkutano ili kuratibu namna vikundi mbalimbali vinavyoweza kuonana. Ama mikutano mbalimbali imekuwa ikihamasishwa na Mhashamu Provencheres, Padre Voillaume na Dada mdogo Magdalena.

Kwa sasa viongozi wa umoja mbalimbali hujaribu kwenda kwa kina kwenye ujumbe wa kaka karoli, wakifanya hivyo ili kuvumbua zaidi utajiri na wingi wa kila kikundi. Kwa vile kila kikundi kimekuwa na chanzo kikuu kimoja cha maisha ya kiroho, tofauti ziwazo hazijalishi bali zinakamilishana jinsi ambavyo upinde wa mvua unavyokamilika kutokana na tofauti ya rangi.

Haja ya kujiunga na familia ya Kaka Karoli imekuwa ikiongezeka kwa miaka sasa. Desemba Mosi imekuwa ni fursa kwa wanachama mbalimbali katika familia za kiroho kila nchi kujumuika na kufanya mikutano. Kumekuwapo pia maonyesho ya shughuli ambazo zinakuwa kielelezo cha maisha ya kiroho ya Kaka Karoli ambayo hushuhudiwa na Kanisa na ulimwengu kwa jumla; ni kama ilivyokuwa wakati ule wa kutangazwa Kaka Karoli ni mwenye heri mnamo 13/11/2005. Familia ya kimataifa huhusika kuratibu mawasiliano.

***Maswali:***

1. ***Upeanaji taarifa umeimarika kiasi gani nchini ama jimboni mwangu ambapo kuna vikundi vya Familia ya kiroho ya Kaka Karoli?***
2. ***Kila aliye mwanachama katika Umoja wa Walei, na kwenye Familia ya kiroho analo jambo la kutoa na kupokea. Bila shaka naalikwa kubaini vipaji vyangu na karama zangu ili niweze kutoa chochote kama sehemu ya mchango wangu. Mchango wangu binafsi ni upi?***
3. ***Nitawezaje kuchangia mawazo katika majadiliano ya wanachama wenzangu?***

# SURA YA TATU

## Wajibu wa Walei

**Mawasiliano yasiyo haririwa baina ya Karoli wa Foucauld na Monsinyori Joseph Hours**

Mei 3, 1912, Assekrem (Ahaggar), Aljeria.

*Monsinyori,*

*Nimeipokea barua yako yenye kubainisha mahitaji yaliopo Ufaransa na nchi zingine zinazohitaji huduma za kanisa; kuna haja ya kuimarisha kazi hasa za walei, jambo ambalo nimekuwa nikilifikiri kwa muda sasa.*

*Tunawahitaji mapadre wenye moyo kama wa Prisila na Akwila ili tufaulu katika kuwaendea wale ambao hatujaweza kuwafikia, kufika katika sehemu ambazo hatujaweza kufika, kuwafikia wale ambao wamemkimbia mbali Bwana, na kuenjilisha kwa njia ya kujenga uhusiano mzuri huku tukifurika wema, tukiwa na pendo ambalo daima ni la kutaka kujitoa, tukiwa mifano mizuri dhidi ya ule ukasisi ambao wengine wamezikimbia huduma zake pengine kwa kukerwa nao ama kwa chuki iliyojengeka dhidi ya ukasisi.*

*Uovu waonekana kujisimika. Bila shaka kunakosekana fadhila kuu, au kama zipo basi zimedumaa. Fadhila hizo ndizo upendo, uvumilivu, upole… Fadhila hizi zimedhoofu na pengine hazieleweki barabara!.*

*Upendo ndio msingi wa dini, nao humfanya kila mkristo aweze kumpenda jirani yake. (Wajibu wetu wa kwanza ni wa kumpenda Mungu, na wajibu wa pili ambao ni sawa na ule wa kwanza ni wa kumpenda jirani kama nafsi yako). Ujumbe huu una maana kuwa kazi ya kumwokoa jirani yako ifanye kama kazi ya kujiokoa mwenyewe! Kwa mantiki hii basi kila mkristo anapaswa kuwa mtume! Huu si ushauri, ni amri ya upendo. Lakini utakuwaje mtume basi? Aha! Kwa njia ile ile ya kawaida tuliyonayo. Walei wanaweza kuwa mitume kwao wote wale ambao wanaweza kuwafikia. Kwanza wataanza kwenye familia zao, halafu kwa watu wa karibu kama marafiki, na kwa vile upendo hauna mipaka, basi watawafikia wale wote ambao wamekumbatiwa na Moyo Mtakatifu wa Yesu.*

*Walei wanaweza wakajitoa kikamilifu endapo watawahudumia wale wote wanaokutana nao kwa sababu tu wema, upendo, fadhila, unyenyekevu na upole vimewasukuma kufanya hivyo. Hivi ndivyo inavyowapasa wakristo kuishi. Wakati mwingine mkristo anaweza asiseme lolote lakini akawa kabisa dada au kaka mwema kwa namna ambayo ameweza kuwa mvumilivu au mwema*

*kama Mungu. Aidha aina za sala zinazotumika ziwe ni zile ambazo watu wote wanazielewa, hata hivyo akitokea mmojawapo anayehitaji ufafanuzi wa kina kuhusu imani basi aongozwe kwa padre kwa maelekezo zaidi.*

*Kila mmoja wetu hana budi kumhesabu mtu mwingine yeyote kama ndugu. "Nyote mko ndugu kwa sababu Baba yenu wa mbinguni ni mmoja." Tukubali kuwa kila mmoja wetu ni mwana wa Mungu, ni roho iliyookolewa kwa damu ya Kristo, ni roho yenye kupendwa na Kristo, ni roho tunayopaswa kuipenda kama tunavyojipenda wenyewe, na ambayo wokovu wake sharti tuuhangaikie. Tuachane na moyo wa uhasama. Kristo alisema "Nawatuma kama kondoo kwenye kundi la mbwa mwitu" Ni ufa mkubwa kiasi gani uliopo kati ya njia zake Kristo na njia za wale wenye kujaa uhasama ambao si wakristo ama ni wakristo wasio wema? Watu wasio wema daima hufikiri kwanza namna wanavyoweza kupambana na maadui wao badala ya jinsi wanavyoweza kuwatendea mema hao maadui zao. Angalia msafiri aliyelala barabarani baada ya kujeruhiwa alihitaji kutendewa wema, je wasio wema si wanaweza wakawa wasamaria wema?*

*Kinachohitajika kwa sasa ni kwa wazazi katika familia zao, mapadre kwa njia ya katekisimu na mafundisho ya dini, na kwa wote ambao kazi yao ni kuwalea na kuwafundisha watoto na vijana, kwamba wachukue jukumu la kuwarithisha watoto na vijana hao kweli hizi za kiimani tangu wakiwa wadogo na kuwakaririsha mara kwa mara ndani ya mioyo yao.*

*Kila mkristo na awe mtume. Hili ni sharti zito la upendo. Kila mkristo amhesabu mtu mwingine yeyote kama ndugu yake mpendwa. Anayeishi dhambini, ni adui wa Mungu, yu mgonjwa kweli kweli. Lakini upendo unatubidisha kuwaonesha wadhambi moyo wa huruma na upendo hata kama wataonekana wamepagawa! Wasio wakristo wanaweza kuonesha uhasama kwa walio wakristo. Hata hivyo mkristo abaki kuwa rafiki mwema kwa kila mtu kwani kila mmoja wetu ana nafasi ndani ya Moyo wa Yesu. Tujifunze kuwa wapole, wenye upendo, na wanyenyekevu kwa wote bila kuvaa hali ya kutaka kupambana. Kristo ametufundisha kuenenda "kama kondoo ndani ya kundi la mbwa mwitu"*[1]

*"Tufanye yote katika yote ili yote yawe kwa ajili ya Kristo. Tutende wema na upendo kwa wote, tufanye kila linalowezekana, tujenge na kukuza urafiki, kwani kwa kufanya hivyo tutawezesha nyoyo nyingi kujongea kwa Yesu.*

*Tusome bila kuchoka Injili ili tuweke akilini matendo, maneno na mawazo ya Yesu na kwa kufanya hivyo tutaweza kufikiri kama Kristo mwenyewe anavyowaza na kutenda. Tufuate mifano na mafundisho ya Yesu, kamwe tusiifuate mifano ya kidunia kwani daima imetupotosha.*

*Kwa kweli hiyo ndiyo dawa pekee ingawaje utekelezaji wake si rahisi kwani unagusa mambo nyeti na ya undani kabisa kimaisha ingawaje mahitaji ya kiroho ni ya wote. Ugumu unakuja kwa vile hatuwezi kuacha mara moja. Hata hivyo jinsi mahitaji yatakavyokuwa yanaongezeka ndivyo tunavyoweza kucharuka na kuamua kuchukua hatua. Mungu daima huwasaidia wanaoonesha*

[1] Mwangwi wa Kaka Karoli: Makala mwanana ya *Maisha ya kiroho* iliyoandikwa na Padre T.R.P. Sertillanges wa shirika la Wadominika, Juni, 1949 tunasoma hivi.
*Jibidishe kuwahudumia wengine kwa wema na uvumilivu. Usipambane na chuki ya kudhania kwa pupa, usije ukayadhuru macho ambayo yangehitajika kufunguka taratibu ili kuona mwanga. Unaweza ukaurarua moyo kwa ajili ya kusahihisha makosa. Unaweza ukalivunja kongwa la dhambi pasipo kulimegua kidogokidogo, unaweza ukaitupilia mbali mioyo yenye kukata tamaa. Makosa na uovu, vinavyosubiri ndani wa moyo wakati mwingine havina madhara sana kama upanga unaorushwa bila busara rohoni kwa lengo la kuikinga.* Ushauri huu umo kwenye *Katekesimu ya Wasioamini*, umejaa hekima na utu. Je hatuoni mwangwi wa mawazo wenye kutupeleka karibu kabisa na Karoli wa Foucalud?

*jitihada. Mungu haachi kumwendea yeyote anayemhitaji. Sisi ndio tusiomtafuta Mungu na hatuonekani kwake. Ikitokea hujafanikiwa kutokana na juhudi uliyoianza, usikate tamaa kwani kwa kuonesha jitihada fulani unashiriki kukamilisha Utashi Mtakatifu hivyo kazana na endelea kuwa mtiifu kwa Mungu…*

*Tafadhali peleka salamu zangu za heshima kwa Padre Crozier mara utakapoweza kufanya hivyo. Na daima tarajia majitolea ya kiroho kutoka kwa mtumishi mnyenyekevu wa Moyo wa Yesu"*

*Kaka Karoli wa Yesu.*

**Chachu kwenye mkate.**

Kwa njia ya ubatizo wakristo wote wanaitwa kuitangaza Injili na kuishi kile walichokielewa kutokana na Injili. Kazi mahususi ya walei ni kuipeleka Injili mahali ambapo kanisa au mapadre si rahisi kufika. Walei tumetapakaa sehemu mbalimbali; tupo maofisini, kwenye biashara, katika shule, kwenye hospitali, sokoni, kwenye mabasi, gari moshi, n.k. Tuko kila mahali! Hivyo uwepo wetu katika sehemu zote hizi unatuwia jukumu kubwa mno- jukumu ambalo Kristo ndiye aliyetukabidhi. Tumeitwa kuwa chachu katika donge. Tumeitwa kuwa chachu katika jamii, katika kanisa na katika ulimwengu.

Imani aliyokuwa nayo mwenzetu Kaka mdogo Karoli wa Foucauld kuhusu walei ilikuwa imevuka mipaka kwa nyakati zake ambapo aliamini kuwa walei wanao mchango muhimu sana katika kueneza Injili. Tukirudi nyuma, mnamo 1912, miaka takriban 50 kabla ya Mtaguso wa Pili wa Vatikano, Kaka Karoli alimwandikia J. Hours kuhusu hitaji la walei katika kueneza ufalme wa Mungu. Walei, jinsi walivyokuwa Akwila na Prisila nyakati za mtume Paulo kule Korintho (Mdo 18: 18-19) wanayo sifa pekee ya kutapakaa katika kila pembe ya dunia kinyume na walivyo mapadre na hivyo kuweza kushuhudia Imani, Matumaini na Mapendo kati ya watu. Kadiri walei watakavyoweza kuonesha kuwa pendo la Mungu limekuwa ndio chanzo cha uhai wa mwanadamu, ndivyo watakavyotakiwa kukubali kuwa wanadamu wote ni wana wa Mungu na hivyo ni lazima kumpenda na kumhesabu kila mtu kama ndugu yetu.

Maneno yatakayofuata yamenukuliwa kutoka kwenye Agano Jipya na yanakusudiwa kutuonesha maeneo ya kazi zetu. Naam, yanatoa maelezo juu ya mipango yetu ambayo haijawa dhahiri. Tunahitaji kwa njia ya jumuiya zetu za kidugu kuelekezana na kujizoeza jinsi ya kuifikia na kuikamilisha mipango yetu. Vivyo hivyo tutakumbana na misamiati muhimu tutakapojifunza kuhusu "Njia ya Pamoja", kadhalika na maisha ya kiroho ya Karoli wa Foucauld. Hivi kwa pamoja vitaboresha sana uelewa wetu juu ya mipango yetu na hivyo kuelewa ni nini cha kufanya.

**UMOJA (KOINONIA)**

Familia zetu kimsingi zinaishi maisha ya kidugu. Wanachama wa maisha ya kidugu wanahimizwa kuzidi kuonesha umoja kwa njia ya kuonesha moyo wa kujali na kushirikishana. Wanachama wanatakiwa wawe mitume wa kueneza wema, uchangamfu, upendo na upole. Chachu huwa kidogo na isiyojaa konzi. Huwezi ukaitambua pindi utakapoichanganya na unga ingawaje hubaki na thamani yake. Kwa njia hii ya kujipenyeza kama chachu kwenye maisha ya watu (unga) ndivyo mabadiliko yawezavyo kutokea. Hata kama idadi yetu ni ndogo, bado tunaweza kuwa alama kabisa ya urafiki na upendo wa Mungu kwa namna tunavyostahili katika uwepo wetu. Hatuhitaji kuhesabu mafanikio yetu yamekuwa kiasi gani kwani neno "mafanikio: si miongoni mwa majina ya Mungu. Donge zima likiumuka, kiasi kidogo cha chachu ndicho kinakuwa chanzo cha nguvu ya maisha.

**HUDUMA (DIAKONIA).**

Yesu, kwa njia ya maisha yake anatufunza kwamba nasi tuwe watu wa kutoa huduma kwa wengine. Huduma zetu zisitawaliwe na ubinafsi na tusihodhi hizo huduma sisi wenyewe tu. Kaka Karoli kwa njia ya maisha yake amedhihirisha na kuonesha kuwa daima amekuwa tayari kupatikana wakati wote kwa kufungua milango kwa wote waliokuwa wasafiri, kuwa mkarimu na rafiki kwa wote bila kujali tabaka, kabila na dini. Kadiri alivyowahudumia hao kwa upendo makini ndivyo ambavyo alizidi kuwa "ndugu wa wote".

Ili kukonga nyoyo za wengine kunahitajika kuwa na sifa za uvumilivu na upole. Yesu kwa kiwango cha juu kabisa alituonesha sifa hizi kwa njia ya maisha yake. Yesu alikuwa mwema na mkweli kwa mambo yanayohusu haki. Leo hii ukitaka kuwa chachu katika donge, chaguo lako lazima liwe kwa masikini, na liwe bayana. Hatuwezi kumuenzi Yesu Kristo kwa kuunga mkono mifumo miovu. Ndivyo alivyosema Kaka Karoli: "Hatupaswi kunyamaa mithili ya mbwa walinzi wasivyoweza kubweka dhidi ya mifumo miovu".

**KUTANGAZA MATENDO MAKUU (KIFODINI)**

Kaka Karoli ananena kuhusu walei kufanya uinjilishaji.  Si rahisi kanisa na walei kwa pamoja kubaini mchango uliopo baina yao katika kuenjilisha. Ili kuweza kufanya kazi bega kwa bega na mapadre wanahitajika akina Prisila na Akwila ambao wanaweza kung'amua kile ambacho mapadre hawajaking'amua au kuweza kwenda mahali ambapo si rahisi kwa mapadre kwenda huko.

Uinjilishaji si lazima uwe ni kutangaza tu neno la Mungu, kunahitajika kuutafsiri katika vitendo ujumbe wa Injili jinsi Yesu mwenyewe alivyofanya. Ili tutangaze habari njema, wakristo wote wanaalikwa kuwa wafuasi wa Yesu. Kumbe tunahitajika kukuza uhusiano wetu na Yesu, kwa kumjua na kumpenda kimatendo. Kwa hiyo wanachama wa umoja wanaalikwa kusoma na kusoma tena Injili na kuishi kulingana nayo. Hili liwe zoezi la kila siku kwani linatujengea uwezo na furaha ya kuishi maisha yanayostahiki.

**KUFANYA SHUKRANI NA KUTUKUZA (LITURUJIA)**

Ekaristi ni sakramenti ambayo haishii katika kuadhimishwa kanisani bali katika maisha yote kwa jumla. Kuadhimisha sakramenti hii kusiishie katika madhabahu tu bali kutangazwe kwa nji ya maisha yetu yote. Maisha yetu yanapaswa kuwa sakramenti
Kwani tumeumbwa kwa mfano wa Mungu.  Maisha yetu yawe maisha ya kuimba sifa na kutoa shukrani kwa Mungu mambo ambayo tunaweza kuyafanya kwa njia ya kupigania umoja, kushiriki mkate na wenye njaa, kuvunjika moyo na wanaoteseka kwa ajili ya kutetea haki.

Walei wasionekane kama nakala au kivuli cha mapadre au wamisionari kwani kila mwanadamu ni kifano pekee cha sura ya Mungu. Kufanana na Mungu ni zawadi, kila mtu ana kipaji chake awezacho kukitoa kama zawadi kwa wenzake. Hii ni changamoto hasa tunapoweza kutambua kuwa kila mtu ni wa pekee na hivyo kuwawezesha wengine kujitambua kuwa kila mmoja wao ni wa pekee pia.

***Maswali***

1. ***Ninaweza kutoa mchango gani katika kupokea na kutangaza ufalme wa Mungu kwenye dunia hii iliyojeruhiwa?***

2. ***Nitaishi maisha gani ambayo yatakuwa ndio ushuhuda wangu wenye matumaini na uaminifu kwa Mungu.***
3. ***Ni kipi cha kufanya ili maisha yangu ya kiroho yazidi kuimarika katika maisha ya Yesu?***

# SURA YA NNE

## UMOJA WA WALEI MAANA YAKE NINI?

**Historia fupi ya Umoja wa Walei**

Kaka Karoli aliubatiza umoja wa kwanza wa walei kwa jina la **"Umoja wa Kaka na Dada wadogo wa Moyo Mtakatifu"** (Machi 11, 1909). Umoja huu aliukabidhi majukumu matatu:

- Kuwarejesha wakristo kwenye maisha yanayoendana na Injili.
- Kukuza upendo juu ya Ekaristi Takatifu miongoni mwa walei.
- Kuletea msukumo thabiti wa kuwaongoa wasioamini.

Katika nyakati hizo, aliwakumbusha walei juu ya wito wao wa kuwa watakatifu na kubeba jukumu lao la kimisionari. Umoja huu ulikuja ukawa kazi yake kuu hasa kwenye miaka saba kabla ya mwisho wa uhai wake. Alizuru Ufaransa mara saba kwa ajili ya kuutangaza na kuufanya umoja huu utambuliwe na kanisa.

***Mchango wa Louis Massignon:***

Wakati Kaka Karoli anafariki, kulikuwa na wanachama wapatao 48 ambao kama si jitihada za Louis Massignon wangesambaratika. Lui alikuwa ni kijana aliyehitimu katika chuo kikuu na alijihesabu kama mrithi wa masuala ya kiroho ya Kaka Karoli wa Foucauld. Waliwahi kusafiri pamoja mnamo 1909 hadi Ufaransa ambamo inasemekana kuwa katika usiku mojawapo waliweza kusali kwenye kanisa la Moyo Mtakatifu huko Montmartre, Paris na kwamba siku hiyo ndipo hasa wazo la Kaka Karoli kuhusu walei lilipata maongozi ya kimungu.

Kaka Karoli alipofariki, Louis aliufufua "Umoja" uliokuwa hatarini kutoweka na ukawa katika hadhi yake na ilipofika 1923 umoja huo ukawa umepewa jina rasmi kuwa ni **"Umoja wa Kaka Karoli wa Foucauld"**. Louis alikuwa amechukua jukumu pia la kumwomba mwandishi mfaransa, Rene Bazin aandike historia (wasifu) ya Kaka Karoli. Kitabu hicho kilichapwa 1921 na wito wa kumfuasa Kaka Karoli ukawa umeguswa watu mbalimbali wakiwemo Padre Rene Voillaume na Dada mdogo Magdalena.

Louis aliweza kuchapisha "mwongozo" ambao Kaka Karoli alikwisha panga kuuchapisha kwa ajili ya wana umoja. Louis aliuchukulia mwongozo huo si kama sheria bali hasa mwongozo wa kiroho. Aliupitia mara kwa mara hadi kufariki kwake.

***Kukua kwa Umoja wa walei***

Umoja ulifanyiwa marekebesho ya muundo wake mnamo 1950 na kupewa jina la Umoja wa Karoli wa Foucauld na ukawa uwajumuisha walei, mapadre na watawa. Umoja huu ulivijumuisha vikundi mbalimbali kikiwemo kile cha Lyon, Ufaransa ambacho kilikwisha anzishwa kabla hata ya vita vya pili vya dunia.

Padre Rene Voillaume akawa amechukua jukumu la kueneza ujumbe wa Kaka Karoli Ni katika kipindi hiki ambapo hotuba na barua za Kaka Karoli ziliweza kusambazwa. Kwa ujumla maandishi hayo yalikuwa ni ujumbe wa maisha ya kiroho ya Kaka Karoli. Hadi mwishoni mwa 1950 viliweza kuchapwa vitabu kama *Ndani mwa mtima wa watu* ambacho kilipendwa sana, *Shajara na kumbukumbu za Karoli wa Foucauld.* Vitabu hivi viliwavuta sana watu kutokana na ujumbe wake.

Mafungo mbalimbali yaliyoendeshwa na Padre Voillaume yaliwapa watu kwa kina ujumbe wa Kaka Karoli na hivyo kuwafanya waimarishe uhusiano wa wanachama na maisha yenyewe ya kiroho. Kutokana na hali hiyo vikundi mbalimbali vilichipuka na wawakilishi wakawa wakikutana huko Tubet karibu na jimbo la Aix-en-Provence nchini Ufaransa. Mafungo yaliyofanyika 1953 yaliweza kuwajumuisha watu wapatao 200 huko Nancy karibu na Ufaransa, ambapo zamani palijulikana kama monasteri ya Wakartusia. Hii ilikuwa ni fursa muhimu sana kwa walei kushiriki katika ibada ya kuabudu ekaristi takatifu, ulizaa ***Umoja wa walei wa Karoli wa Foucauld*** mwaka 1955 na kuanzia hapo umekuwa ni umoja wa walei. Kadhalika mwaka huo huo nchini Aljeria, Beni-Abbes, ulianzishwa ***Umoja wa Jumuiya za Kidugu za Kaka Karoli wa Yesu***. Umoja huu uliwajumuisha kwenye familia moja vikundi vyote vya walei, watawa na mapadre ambao walijawa shauku ya kunemeka na utajiri wa maisha ya kiroho wa Kaka Karoli. Baadaye umoja huu ulikuja kujulikana kama ***"Umoja wa Familia ya kiroho ya Kaka Karoli wa Foucauld"*** na mkutano wake wa kwanza ulifanyika Tre Fontane, Italia 2003.

***Kukua kwa Umoja wa Walei katika ngazi ya kimataifa.***

Mawazo ya kwamba siku moja 'tuishi kama Kaka Karoli alivyoishi huko Nazareti' na yale ya 'kuishi maisha ya kidugu kwa wote' yaliwafanya baadhi ya walei waliokuwa wamejiunga kwenya jumuiya za ulaya wadhamirie kujihusisha na nchi za katika dunia ya tatu hasa katika Afrika ya Magharibi (Maghreb), Afrika kwa ujumla, Amerika ya Kusini, na hivyo kuwa na mshikamano nao katika kushughulikia masuala ya haki za kibinadamu. Kichocheo kikubwa kilitokana na mapinduzi yaliyomg'oa Pinoke nchini Chile ya 1973.

Hata hivyo kwenye miaka ya 1950 jumuiya za walei zilikuwa zimekwisha anzishwa na kushamiri katika nchi nyingi zikiwemo Ajentina, Brazil, Chile, Kolumbia, Ubelgiji, Hispania, Ureno, Italia, Amerika na Kanada. Walei katika nchi hizi ndio waliowezesha kufanyika mikutano ya kimataifa. Mkutano wa kwanza ulifanyika Marseille, Ufaransa mnamo 1964 ambapo walihudhuria wawakilishi kutoka mataifa kumi na moja. Kuanzia hapo mikutano ya kiwango cha kimataifa imekuwa ikifanyika kila bada ya miaka sita.

***Mikutano ya kimataifa ya Umoja wa Walei***

**1964 Marseille, Ufaransa:** Ajenda ziliweka mkazo juu ya mambo yaliyohusu miundo, kanuni na maisha ya kiroho. Jumuiya mbalimbali za umoja wa walei ziligawanywa katika makundi matano, Kundi la Ulaya ya Kaskazini, Ulaya ya Kusini, Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini, Asia na Afrika. Wasimamizi walichaguliwa kwa kila bara na kwa pamoja waliunda ***Kamati Kuu ya Umoja wa Walei***.

Kanuni mpya kuhusu umoja wa walei zilichapishwa katika kifaransa na kujulikana kama *mwongozo*, baadaye zilitafsiriwa kwenda katika lugha mbalimbali..

1970: Assisi, Italia (Wajumbe 17): Mkutano huu uliweka azimio la kiutendaji. Matumizi ya maneno "Timu ya Kimataifa" badala ya maneno "Kamati Kuu" yaliafikiwa kwa upande wa uongozi.

1976 Tarbo, karibu na Lurdi, Ufaransa (Wajumbe 18): Mjadala nyeti ulifanyika kubaini namna jumuiya za kidugu zilizo nje ya ulaya zinavyoweza kushiriki kikamilifu kwenye umoja wa walei. Benedito Prezia wa Brazil alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu ili kuongoza umoja wa walei. Hii ni kama njia ya kuwathamini wasio Waulaya..

1982 San Cugat, karibu na Baselona, Uhispania (Wajumbe 16): Wajumbe walikazia nafasi ya watu maskini kwenye umoja wa walei, namna wanavyoweza kushiriki kazi na kuwa wanachama. Waraka mfupi uliojulikana kama "Njia ya Umoja" ulitayarishwa kufafanua mambo yanayounda umoja wa walei na uhusiano uliopo baina ya sala na majukumu, huu ndio umekuja kuwa nguzo kuu ama *Carta Magna,* kwenye maisha ya umoja wa walei. Wanachama kutoka jumuiya za Ubelgiji walichaguliwa kuunda timu ya kimataifa.

1988 Natoye, karibu na Namur, Ubelgiji (Wajumbe 27): Timu ya kimataifa iliundwa kutoka wawakilishi wa kwenye nchi mbalimbali duniani.

1994 Orsay, karibu na Paris, Ufaransa (Wajumbe 27): Timu ya kimataifa yenye wawakilishi kutoka kila bara. Rene Haentgen wa ubelgiji akachaguliwa kuwa Mratibu Mkuu.

2000 Araruama, karibu na Rio, Brazil (Wajumbe 24): Huu ulikuwa ni mkutano wa kwanza wa kimataifa kufanyika nje ya bara ulaya. Ajenda ilikuwa "Mungu anaumba upya ulimwengu". Zaidi ya washiriki 100 walijumuika. Amerika ya Kaskazini na Kusini walijumuika kuwa bara moja, wakajulikana kama waamerika. Timu mpya ya kimataifa ikawahusisha wawakilishi kutoka kila bara, yaani Ulaya, Afrika, Asia, Arabia na Waamerika. Katibu Mkuu mpya akachaguliwa ambaye ni Mariana Bonzelet wa Ujerumani.

2006 Arusha, Tanzania. Mada kuu ilikuwa "Fikra za kitume na kinabii kwa walei wana umoja"

## 4.2. "NAMNA YA KUISHI KATIKA UMOJA"

*(Maandishi yalijadiliwa na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Walei huko San Cugat (Barselona), Hispania, mnamo Agosti 1982, na kuhaririwa na Mkutano Mkuu wa jumuiya za umoja wa walei huko Araruama (Rio de Janeiro), Brazil, 29 Julai, 2000).*

### I. UMOJA WA WALEI

Ni mjumuiko wa wanawake na wanaume wa rangi na matabaka, mbalimbali, ambao kwa kufuata mfano wa Karoli wa Foucauld, hudhamiria kusaidiana wao kwa wao katika kumfuasa Yesu Kristo na katika kuishi Injili. Umoja huu kimsingi ni kwa ajili ya wakatoliki, hata hivyo yeyote asiye mkatoliki anaweza kujiunga maadamu amevutiwa na ujumbe wa Kaka Karoli.

### II. ARI

Wanachama kwa kuzingatia mawazo ya Kaka Karoli, hualikwa kuishi maisha ya kutojulikana hadharani ya Nazareti ambayo kimsingi huzingatia.

a) Kumtafuta daima na kumpokea Yesu aliye mwana wa seremala ambaye kwa hakika ni Mwana wa Mungu aliyejifanya mwanadamu.
b) Kuitangaza Injili kwa njia ya maisha yao.
c) Kushikamana na maskini ambayo ni ishara ya uwepo hai wa Kristu miongoni mwa wanadamu.
d) Kuleta umoja na uhusiano mwema kati ya makanisa, dini na watu wa mataifa yote duniani.

1. Hamu ya wana umoja kuyafanya maisha yao yamfanane Yesu Kristo itatambulika kwa njia ya:
a) Uwepo halisi wa Mungu ambao huonekana kwa kumwabudu Yeye katika Ekaristi Takatifu.
b) Kumkaribisha Mungu kwa njia ya Neno lake hasa kupitia Injili.
c) Kumtafuta Mungu kwa njia ya sala za binafsi, mafungo, "siku za kuwa jangwani", na kwa kujiachilia mikononi ya Mungu.
d) Kujitahidi kukutana na kumpenda Mungu kwa njia ya kuwahudumia watu wote.

2. Ili kujishikamanisha na watu maskini, wana umoja hujaribu kufanya yafuatayo:
a) Kuishi maisha ya kawaida kwa kuhiari maisha ya wanaoishi 'alimradi mkono uende kinywani'.
b) Kushirikishana huzuni, matumaini na kutokuelewana ili kuweza kutafuta uhuru wa kweli.
c) Kuweza kuwapenda watu wote wakiwamo majirani hasa waliotelekezwa na kuyashughulikia mahitaji yao ya kimwili, kiroho na kuwapa moyo kwa jumla.

3. Kwa njia ya maisha yao wana umoja wanaalikwa kuwa:
a) Kuwa na uelewano na upendo na kuguswa na hitaji la kila mmoja wao.
b) Mabadiliko ya dhati ambayo yatafanyika kutokana na kuyaangalia upya maisha ambapo kila mmoja hana budi kujipekua ndani ya maisha yake binafsi na kwenye uhusiano wake na watu wengine na kuona ni kwa kiasi gani amefanikiwa kuishi Injili.
c) Kuhiari kushiriki mahitaji binafsi ili kupata mahitaji ya pamoja ambayo matumizi yake yanasimamiwa na jumuiya.

4. Umoja ufanye kila linalowezekana na bila ya kuathiri maisha ya wanachama, kukabiliana na mazingira ambapo haki za binadamu zinakandamizwa.
5. Kaka Karoli awe muhimili wa mabadiliko yoyote ndani ya wanaumoja. Wanachama watadumu kiaminifu endapo watazingatia elimu inayotokana na maisha ya Karoli, maandiko yake, na maisha yake ya kiroho ambavyo ndivyo vyombo vya kuwawezesha kudumu katika wito wao na wajibu wa kuishi jinsi Injili inavyoagiza.

## III. UTARATIBU

Umoja huu umeundwa kutokana na mjumuiko wa vikundi vidogo vidogo kwenye mahali husika.
1. Kila nchi inakuwa na 'timu ya kitaifa' ambayo huwa na jukumu la kuviunganisha na kuviwezesha vikundi vyake. Inapowezekana, Padre mmojawapo wa wana timu awe ni padre ambaye ni mwana familia ya Kaka Karoli.
2. Kila nchi inakuwa na utaratibu wake ili kukidhi mahitaji na mazingira yawayo, lakini ni lazima kubaki daima waaminifu kwa mtizamo wa Kaka Karoli na kuendelea kuwa wamoja chini ya timu ya kimataifa.

3. Umoja unaelewa shida zinazowafanya baadhi ya wanaumoja wasiweze kushiriki kwenye mikutano mara kwa mara, ingawaje wanapenda kufuata mwongozo wa namna ya kuishi kwenye umoja wenyewe na maisha ya kiroho ya familia ya kiroho ya Kaka Karoli.
4. Kila bara sharti liwe na utaratibu wa eneo lake ili kukuza ushirikiano na majadiliano.
5. Mkutano Mkuu utafanyika kila baada ya miaka sita.
6. Mkutano Mkuu una makusudi yafuatayo:

a) Kuandaa mkutano kwa ajili ya wawakilishi kutoka kila nchi.
b) Kutenda, kusali, kusikiliza na kuamua kwa pamoja.
c) Kuamua lililo sahihi na lipi lisilo sahihi kulingana na mpango wa wanaumoja.
d) Kuchagua timu ya kimataifa itakayodumu kwa miaka sita. Ni vizuri timu ikawa na padre mwana umoja, tena ni vizuri wakawepo wanachama wawili au watatu ambao ni wanachama wa sasa au wenye kufahamika na mkutano mkuu.

Timu ndiyo itakayokuwa alama ya umoja kati ya wanaumoja wote na ndiyo yenye jukumu la kuwezesha, kutia moyo ili mshikamano uzidi kukua na kuenea duniani pote.

7. Umoja ufanya mawasiliano ya mara kwa mara na matawi ambayo ni wanafamilia ya kiroho ya Kaka Karoli, na hasa kwenye jumiya kuu ya Wanaumoja wa Kaka Karoli wa Yesu.

### 4.3. **Umoja wa Walei Pande zote za dunia**

Orodha ifuatayo inazingatia mgawanyo wa mabara kwa mujibu wa jumuiya za umoja.

AFRIKA

Benin
Burkina Faso
Burundi
Kameruni
Jamhuri ya Afrika ya Kati
Kenya
Madagaska
Niger
Jamhuri ya kidemokrasi Kongo
Rwanda
Sierra Leone
Tanzania

AMERIKA

Ajentina
Bolivia
Brazil
Chile
Kolumbia
Kosta Rika
Kyuba
Ekwedo
Haiti
Meksiko
Peru

UARABUNI

Aljeria
Misri
Irak
Jordan
Lebanoni

ASIA

India
Japan
Pakistan
Filipino
Kores ya Kusini
Sri Lanka
Vietnam
Australia

ULAYA

Ubelgiji
Uingereza
Ufaransa
Ujerumani
Hangari
Ireland
Italia
Malta
Uholanzi
Poland
Ureno
Hispania
Switzerland

# SURA YA TANO

## MAISHA KWENYE JUMUIYA YA WANAUMOJA

Maelekezo yafuatayo hayakusudiwi kuwa sheria bali yawe ni mwongozo. Jumuiya zilizo katika ngazi za chini zizingatie hali ya kimaisha ya kila mwanachama. Mathalani, zitakuwepo tofauti miongoni mwa wanachama kwa vile watakuwepo ambao ni vijana, watu wazima, wenye ndoa na wasio na ndoa, kuishi kwenye mazingira tofauti, n.k. Ndani ya umoja. hakuna atakayehukumiwa kwa lolote zaidi ya kila mmoja kuwajibika juu ya maisha yake ya kiroho

**Uanachama**

Mwanachama anaweza kuwa
- Mwanamke au mwanamme
- Aliye au asiye oa/olewa
- Wanafamilia pamoja na watoto na vijana wao.
- Mapadre na watawa.

Wanachama watatofautiana kwa umri na kazi wanazofanya. Wanachama watatofautiana kwa kabila na hata mfumo wa kimaisha. Mahitaji ya watoto yazingatiwe ingawaje watoto hawawi mara moja wanachama kwenye umoja.

*"Umoja ulianzishwa ndani ya Kanisa Katoliki, lakini sasa umefungua milango kwa wale wote wanaohiari kuufuata ujumbe wa Kaka Karoli".*

Sasa kuna fursa zaidi za uekumene yaani kuweza kushirikiana na watu wa imani mbalimbali kwa kufanya nao mikutano yakiwemo Makanisa ya Mashariki, na makanisa mengine ambayo ni ya Waluteri, Waanglikani na Waorthodoksi. Mazungumzo baina ya dini kuu kama vile dini ya Kiyahudi, Kiislam na Kibudha pia yanaweza kufanyika.

Umoja mahalia: Kikundi kiwe na wanachama wachache tu, kati ya watatu hadi kumi na watano ili kumwezesha kila mmoja kufanya tafakari halisi kuhusiana na maisha aliyonayo. Hata hivyo vizuri kikundi kigawanyike kinapokuwa na wanachama 10 ili kuwa na vikundi viwili kwa ajili ya kurahisisha majadiliano. Endapo kuna wasio wanachama lakini wanamoyo wa kupenda kujua yanayojiri katika umoja mahalia, wanaweza kukaribishwa na kushiriki kwenye majadiliano.

Ahadi ya kujitoa kikamilifu kwenye umoja wa walei yaweza kutendeka wakati wa mojawapo ya matukio ya kijimbo ama kitaifa. Uadhimishaji wa pamoja hadharani huleta hisia za kuunganika na jamii pana zaidi ya kimataifa.

**5.2. Uanachama 'pweke'**: Hawa ni wale ambao awali walikuwa wanachama lakini kutokana na sababu za ugonjwa, umri, masuala ya kifamilia, umbali, n.k. wanashindwa kujumuika na kushiriki kwenye umoja mahalia lakini bado wana moyo wa kufanya hivyo. Baadhi yao huendelea kuishi maisha ya kiroho ya Karoli wa Foucauld. Na wanatoa ushuhuda mkamilifu mathalani kwa kushiriki katika mikutano ya kijimbo au ya kitaifa kadiri wanavyoweza.

Umoja mahalia udumishe mawasiliano na wanachama 'pweke' kwa mojawapo ya njia hizi:

- Taarifa zilizoandikwa, naswa sauti au za kuonwa: Hizi ni pamoja na majarida ya kitaifa, barua, video, simu, kanda, n.k.
- Ujirani mwema: Kutembeleana kati ya wanaumoja, kuhusishwa na majukumu ya kitaifa, n.k.
- Mialiko na mipango itakayowawezesha kushiriki katika hafla maalum za wana umoja kama vile ‘sherehe za Desemba Mosi, n.k.

**Wajibu wa vijana.**

Umri wa kuwa kijana hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kwa vile umri kati ya miaka 25 hadi 40 huhesabika kama rika la utu uzima, bila shaka vijana tunaowazungumza hapa ni wale wenye kuwa na miaka kuanzia 16 hadi 25. Hawa waunde jumuiya zao za kidugu tofauti na za watu wazima, kwa sababu;
- Ni rahisi kushirikishana mawazo na mahitaji.
- Hupendelea kukutana na wenzao mbalimbali walio katika umri sawa na wenye mahitaji yanayofanana.
- Desturi na mila zetu huhitaji faragha hasa wakati wa majadiliano
- Mwelekeo wa vijana kufanya tafakari hutofautiana na wa watu wazima, mfano kukaa kimya kwa vijana kuna maana tofauti na kwa wazee.
- Hupenda kujimudu katika utendaji wao.

Jumuiya za umoja za vijana wakati mwingine hujumuisha wanafunzi ama watoto ambao wazazi wao ni wanachama. Ni muhimu vijana kama hao wakitamka wao wenyewe kwamba wanashiriki kwa kuhiari yao.

**Mikutano ya wana umoja mahalia: Lengo**

Wanaumoja, kwa kuishi alivyofanya Kaka Karoli, wataweza kuwa msaada kwa kila mmoja wao wakati wanapokutana kwa njia zifuatazo:
- Kumfuasa Yesu Kristo na kuishi Injili ulimwenguni.
- Kuishi kama dada na kaka wa Yesu
- Wamshuhudie Kristo katika maisha ya kidunia
- Wawe wakarimu kwa watu hasa walio wahitaji, waliotelekezwa, wasio na matumaini, watu duni na waliotengwa na jamii.
- Waishi maisha ya unyoofu (Maisha ya Nazareti)
- Wawe chembe hai ya kanisa.

**Ratiba**

Vikundi vikutane kila mwezi ingawaje ratiba ya kukutana mara kwa mara inaweza ikatengenezwa na wana umoja mahali. Mikutano iwe ni chanzo cha manufaa mbalimbali badala ya kuonekana kama mzigo. Shughuli binafsi za wanachama zisiathiriwe na ratiba za mikutano ndio maana pendekezo la kufanya mkutano mara moja kwa mwezi lawezekana kwa kila kikundi.

Wakati wa kufanya mikutano weza kuwa katika mojawapo ya saa za jioni, siku nzima mojawapo au siku mojawapo mwishoni mwa juma.

**Ajenda au mada**

Yafuatayo ni mapendekezo ya mambo ambayo yanaweza kujadiliwa ingawaje hakuna sharti la kutokuwa na mada nje ya hizi. Uchaguzi wa kuzizungumza mada zote au sehemu ya hizo mada unategemea namna kikundi kitakavyoweza kuweka uwiano kati ya sala, ushiriki wa wanachama na mvuto wa majadiliano.

Mungu hapendezwi na ‘nidhamu ya kondoo’ bali anataka ushiriki wa kikamilifu kwa kila mmoja kwa akili, roho na mwili.

Mapendekezo ya mada kwa ajili ya mikutano:

- Kubadilishana uzoefu kutokana na maisha tunayoishi katika familia, kazi zetu, ushiriki wetu katika masuala ya kijamii au siasa, n.k.
- Kusikiliza na kutafakari pamoja Neno la Mungu.
- Sala
- Tathmini ya maisha
- Kuabudu
- Ekaristi
- Kuzama kwenye maisha ya kiroho ya kaka Karoli
- Kuwa na mlo wa pamoja, burudani, sherehe, n.k.

***Kujali maisha ya kila mwanachama*** ni jambo la maana kwenye mikutano ya wana umoja mahalia. Maisha ya kiroho yanaunda sehemu muhimu kwenye maisha ya kila mmoja na yanaundwa na mihimili miwili; kazi na tafakari. Wanachama kwa kushirikishana maisha yao watajikuta wanatathmini maisha yao na kuyafanya upya, hasa wakiongozwa na Injili na maandishi kutoka Kaka Karoli (Rejea 5.5)

***Kuabudu Ekaristi Takatifu*** inawezekana kusifanyike mara kwa mara, lakini sala daima zinawezekana kufanyika. Padre anapokuwepo ni dhahiri adhimisho la Ekaristi lawezekana. Utaratibu wa kuabudu ekaristi unaweza kufanyika kwenye kanisa la parokia iliyo karibu. Adhimisho linapokuwepo wanachama kutoka jumuiya za jirani wanaweza kualikwa na kushiriki katika kuabudu.

***Kujitambua*** ni jambo muhimu, ni muhimu kuwa na fursa za kushiriki katika burudani mbalimbali. Kikundi kinapopata nafasi ya kujumuika ni vizuri pia watoto, ndugu na jamaa wakashirikishwa. Kikundi chaweza kufanya hivyo jioni mojawapo au katika mwisho wa wiki.

Kitu muhimu kinachotufanya tujumuike ni ***uhusiano*** wetu na Yesu, uhusiano wetu na wanachama wenzetu na wale wote tunaoishi nao. Maisha ya kidugu yanataka kuwako mtizamo wa kuwasikiliza wengine kwa makini na ufasaha.

### Majitoleo kamili kwenye uanachama wa umoja wa walei

Kila mwanachama wa umoja atajitoa kikamilifu kulingana na vipaji alivyojaliwa. Majitolea ya wanachama yatathminiwa kwa kuongozwa na mwanga wa Injili na hivyo kupewa changamoto mpya kutokana na michango ya mawazo ya wana umoja mahalia. Kila mmoja akijitoa na kuishi kwa uwazi kwa nia ya kujiweka tayari kutoa huduma, wana umoja kwa kufanya hivyo wataweza kuonesha mshikamano wao hata katika hatua za kuelekea kukata tamaa. Kwa kila mmojawapo wa wanachama atachagua kushiriki katika huduma fulani kama mchango wake kutokana na karama alizojaliwa. Kwa kufanya hivyo jumuiya itakuwa na utajiri wa karama na wingi wa huduma.

Jumuiya isinyamae katika masuala ya kijamii yenye kujawa na matatizo. Tukumbuke Kaka Karoli hakuwa amependa kubaki kama ‘mbwa mlinzi asiyependa kubweka’ wakati ule yalipokuwako matatizo yaliyotokana na kuwako biashara ya utumwa. Vile vile wana umoja wasiyafumbie macho matatizo kama vile uhamiaji haramu, msamaha wa madeni ya nje ya nchi za ulimwengu wa tatu, masuala ya vita na amani, ubaguzi, haki za binadamu, n.k.

### Umoja nyakati za mikutano

Ni katika mikutano ambamo wanaumoja kutoka jumuiya ambazo kwa sababu za kijiografia si rahisi wao kukutana, hupata wasaa wa kukutana. Hata hivyo njia za mawasiliano zikiwemo simu, matini, barua, barua pepe, n.k. zaweza kukuza mawasiliano. Pamoja na hayo njia iliyo madhubuti zaidi ni sala, ingawaje mikutano huwa mirefu na yenye kuchosha, bado kwa njia ya sala mwendelezo wa kumpelekea Mungu mahitaji ya watu, majitoleo, mahangaiko na furaha unafanyika. Kuhabarishana yanayojiri kwenye mikutano huimarisha urafiki unaotokana na kuwasiliana huko. Ingawaje umoja mahalia ndio unaokuwa chemchem ya maisha yetu lakini tusijifunge sisi kwa sisi bali tujifunue na kujishikamanisha na wana umoja mahalia kote kote waliko.

### Kufanya mikutano na vikundi vingine ambavyo ni jumuiya ya Karoli wa Foucauld.

Kila Desemba Mosi, huwa ni siku ambamo jumuiya zote huadhimisha kifo cha Kaka Karoli. Hafla hii pia hutumika katika nchi na majimbo kadhaa kujizamisha zaidi katika kujengana juu ya maisha ya kiroho kulingana na ujumbe wa Kaka Karoli. Kila tawi hudiriki kudhihirisha wanavyomshuhudia Yesu wa Nazariti na hasa katika jambo bayana linalogusa ujumbe wa Kaka Karoli. Hafla za namna hii ndizo pia ambako mikutano huandaliwa kwa ngazi za kitaifa na hivyo kuziwezesha jumuiya za kiroho za Kaka Karoli kushiriki. Utaratibu huu unapofanyika unatuwezesha kujiridhisha wenyewe kikamilifu sisi ni akina nani na vipi tutalishuhudia kanisa kwenye jamii tunazoishi. Mada na taarifa kutoka matawi mbalimbali huwasilishwa ili kuwaimarisha wote.

### Mshikamano wa wanaumoja

Mshikamano wa wanaumoja hutoa fursa bora ya kubadilishana uzoefu, kuonana, kudumisha mshikamano na urafiki baina ya jumuiya kutoka nchi na majimbo tofauti. Aidha ni bahati pekee kwa wanaumoja mahalia, kwani kujumuika kwao kunakuza heshima kwa njia ya kupeana habari, mawazo, maandishi, ili mradi kujengana katika maisha ya kiroho ya ki- Foucauld.

Kwa kushikamana hatumaanishi kuwepo kundi moja au zaidi linalofadhili wengine kila kitu na hivyo kujenga dhana tegemezi, hapana! Sote tunapaswa kujengana, kuwezeshana na kusaidiana, hivyo tusiwe namtazamo kwamba zitakuwepo jumuiya za walionacho na nyingine za wasionacho; yatubidi wote tuwe na mwelekeo wa kutoa na kupokea. Katika uhusiano wetu huu tujali kuthamini na kukuza heshima yetu wote kulingana na miongozo ya Kaka Karoli. Matumizi ya mali tulizonazo kwa pamoja ni jambo la ziada. Tuzingatie zaidi mitazamo sahihi na yenye kujenga kwa misingi ya mali tulizonazo ndani ya mshikamano wetu.

Mshikamano waweza kuwako kwa wanaumoja kati ya nchi za bara moja ama nchi za mabara tofauti. Masuala yanayotuweka kwenye mshikamano yawe ni yale ambayo tunayahitaji. Tayari, huko Ulaya, baadhi ya nchi zimeshakuwa na mshikamano, hiyo pekee haitoshi ni budi kuwako utaratibu mzuri unaogawa majukumu na kurahisisha upeanaji taarifa ili kuepa kurudia rudia mambo yale yale kila mara.

### Vijarida na taarifa rasmi

Hivi ni vyombo muhimu vya kuwawezesha wanachama kuanzisha, kushirikishana, kutambua na kuimarisha ujumbe wa kiroho wa Kaka Karoli. Kuna majimbo yenye vijarida ambavyo huandikwa na nchi mbalimbali kwa kupeana zamu, mfano ni huko Ufaransa.

Jarida la kimataifa kwa ajili ya wana umoja wote hutolewa mara mbili kwa mwaka kwa lugha za Kiingereza, Kihispania na Kifaransa. Makala zenye kuwa na umuhimu zaidi hutafsiriwa kadiri ya lugha zinazotumika kwenye majimbo husika. Hii ni fursa ambako habari zinamfikia kila mtu katika lugha yake. Kila jimbo liwe na atakayehusika kutuma makala ama habari kwenye jarida la kimataifa yakiwemo masuala yahusuyo mang'amuzi, mawasiliano na taarifa mbalimbali; na mtu huyo ndiye atakayeshirikiana na mratibu wa jimbo kufanya tafsiri na kuzisambaza.

**Kuleta mwamko wa uanachama katika umoja.**

Ni muhimu kuacha milango wazi ili jamii za wanaumoja ziweze kutia uhai kwenye uanachama. Njia zifuatazo zaweza kutumika:

- Kuwakaribisha wenye moyo ili kuona yanayofanyika kwa kutumia mialiko ya kuja kushiriki katika mikutano ya kijimbo, kitaifa au ya umoja mahalia.
- Kuwalika waamini waje kushiriki katika ibada za kuabudu ekaristi takatifu ambazo zinaweza kupendekezwa kufanyika katika parokia yoyote.
- Maadhimisho ya Desemba Mosi, watu wengi wanaweza kukaribishwa na kualikwa kuja kushiriki katika umoja wa walei.
- Kuwakubali waliotayari kuja na kujiunga.

Hata hivyo muda utahitajika hadi kuweza kumbaini atakayestahili kujiunga. Tusiharakishe kujipatia kundi kubwa kabla hatujaweza kuwatathmini wanaotaka kujiunga. Tunahitaji muda wa kuweza kubaini kama kweli huyu tunayemhitaji Mungu ndiye atakuwa amemwalika kujiunga na umoja wa walei. Umoja mahalia ni kama familia, huhitaji maisha kamili, kuwa makini kwa mahitaji ya vijana, na kuwa wa wazi kwa wanaotuzunguka. Umoja mahalia unapofikia hatua ya kuwa na wanachama wengi, hauna budi ujigawe ili kuruhusu kukua na kuongezeka. Wanachama wakongwe wasikosekane kwenye jumuiya mpya ambazo zimejigawa.

5.11 **Wanaumoja – shina la Kanisa.**

Kama asemavyo Mtakatifu Agustino kuwa Upendo wa kidugu watoka kwa Mungu na ni kwa ajili ya Mungu. Ili kuweza kuwa kanisa ni budi kuonesha mapendo ya Mungu kwa wote. Mungu anatuita ili tuwe sura inayoliwakilisha kanisa kwa wote tunaokutana nao. Mwongozo wetu wa maisha (Kuishi maisha ya Nazareti) ni wa maisha ya kanisa. Wote tunawajibika kujenga kanisa ambalo msingi wake ni Injili, ambao tunazidi kuwa wamoja na kushikamana na wahitaji. Ndani ya maisha ya umoja wetu tugundue ishara muhimu kimaisha kama vile kugawiana vitu, ukarimu, vicheko, mazungumzo, na kuwa wawazi. Kwa njia ya umoja tunazidi kujongea katika hali ya kuwa na dada na kaka katika mataifa yote.

**5.12 Jukumu la Padre**

Padre ni ndugu mwingine mwenye kushiriki maisha ya wana umoja. Nafasi yake kama padre ijawe na unyenyekevu ili aweze kutoa huduma vizuri kwenye umoja anaoshiriki.

Katika ngazi ya kitaifa na ya kimataifa Padre anabeba jukumu pekee la kuadhimisha Ekaristi Takatifu kwa kujumuika na Kanisa kulingana na maisha ya kiroho ya Kaka Karoli. Kwa njia ya kuishi upadre wake ajiwezeshe na awawezeshe anaowahudumia kuimarika kiroho. Ingawaje mwunganiko na kanisa huja kwa njia ya ubatizo, kipaimara na ekaristi, padre kwa namna ya pekee ni binadamu aliye kiungo rasmi baina ya kanisa mahalia na kanisa la ulimwengu. Mapadre wataishi kulingana na kanuni zinazotawala kwenye mabara ama majimbo walimo.

# SURA YA SITA

## Utekelezaji

### 6.1. **Jinsi ya kuanzisha umoja mahalia**

Haipo njia moja tu ya kuanzisha umoja mahalia, hata hivyo ni muhimu kuchanganua na kutekeleza mojawapo ya mapendekezo haya:

- Kwa wanaoishi tayari kulingana na maisha ya kiroho ya Kaka Karoli:
  - Waalikwe ili kujiunga na umoja mahalia.
  - Kuwawezesha ili wajiunge na wenzao waliotayari na waanzishe umoja mahalia.

- Kwa wale ambao wamekuwa wakiyaishi maisha yawayo ya kiroho lakini si yale ya ki-Karoli:
  - Waandaliwe fursa ya kufahamishwa maisha ya kiroho ya Kaka Karoli.
  - Wapewe taarifa kwa njia ya kijarida cha kitaifa cha wana umoja, picha, video, au taarifa zozote zinazohusu maisha ya kiroho ya Kaka Karoli.
  - Waalikwe ili kufahamishwa umoja wa walei ni nini.
  - Pindi fursa hizo zinapotokea. Waalikwa wahamasishwe kuanzisha umoja, chini ya uwezeshaji wa mwana umoja mmojawapo.

- Kwa watakaohitaji kushibishwa maisha ya kiroho:
  - Waalikwe siku yanapofanyika mafungo, hizo ndizo siku za kuwa jangwani.
  - Kwa njia ya fursa hii, hamasa itolewe panapowezekana ili waalikwa weweze kuanzisha umoja.

- Kwa vikundi vinavyohitaji kuwezeshwa na wana umoja
  - Vikundi vijihusishe kwanza kuuelewa umoja unajihusisha na nini halafu taratibu waone nao pia wataanza kushiriki katika mambo yapi.

Namna yao ya kuanza kujihusisha ibainishwe wazi. Kwa kila hatua ni muhimu kuzingatia maisha ya kiroho ya Kaka Karoli na maisha katika umoja. Jambo la muhimu vile vile ni jinsi kikundi kitakavyowezeshwa na jinsi wanaumoja watakavyokilea kwa muda maalum utakaotajwa. Mara kwa mara hatua zifanyiwe tathmini. Msaada huu utategemea kama jumuiya inayobeba jukumu la kukiwezesha kikundi itakuwa iko karibu kiasi gani. Endapo jumuiya haipo karibu basi jukumu la uwezeshaji lifanywe na Kaka wadogo, Dada Wadogo au Umoja wa Walei ulio jimbo jirani.

Uzoefu unaonesha kuwa msaada mkubwa kwa vikundi vinavyoanza hupatikana kutoka kwa Wanafamilia ya kiroho ya Kaka Karoli, Dada Wadogo, Kaka Wadogo, Umoja wa mapadre "Upendo wa Yesu", na umoja wa Walei. Msaada unatokana na ushuhuda wa wana umoja wenyewe kimaisha na jinsi wanavyowatia moyo wanavikundi.
Pindi inapobainika kuwa wapo wanaohitaji kuwa wana Umoja wa Walei, rejea utaratibu uliopo katika sura ya 5.12 "Kurudia Uanachama wa Umoja" na 5.2 "Uanachama pweke". Wahitaji wapewe anwani yenye maelezo kamili.

### 6.2 Jinsi ya kuendesha mkutano wa wanaumoja mahalia.

Ufafanuzi ufuatao unahusu vipengele vya mkutano ambavyo tayari vimetajwa katika sura ya **5.6.** Ni muhimu kuzidi kusisitiza juu ya vitu vitatu hasa: sala – tafakari – ukunjufu wa moyo. Ili mkutano ufanikiwe utategemea jinsi uwekaji mipango ulivyo. Baadhi ya vikundi hupendelea kuwa na chakula cha pamoja kabla ya mkutano, wengine huweza kuanza na ibada ya kuabudu Sakramenti Kuu, wengine

huanza kwa kupeana taarifa mbalimbali, wengine huanza kwa kupata ufafanuzi kuhusu sehemu ya Injili mojawapo au maandiko ya Kaka Karoli. Wengine huanza kwa hujishughulisha na mada mahsusi, au swala linalojitokeza kiutendaji, n.k.

Hata hivyo mikutano ya wanaumoja imetawaliwa na mambo makuu mawili:

- Upeanaji taarifa miongoni mwa wanachama.
- Kuielewa na kuishi Injili.

**6.3 Jinsi ya kumegeana Injili**

**6.3.1 Umuhimu wa peke wa Injili kwa Kaka Karoli**

Jambo la maana ni kumfuasa Yesu wa Nazareti. Tunaalikwa kumkaribisha Roho Mtakatifu afanye kazi ndani yetu. Ili kuweza kuyaishi maisha ya Kikristo na kumdhihirisha Mungu kwa watu, hatuna budi kujishikamanisha na maisha aliyoyaishi Kristo kadiri yalivyo kwenye Injili. Katika mwongozo wa Kaka Karoli tunasoma: *"Jiulize kwa kila jambo: 'Angelikuwa ni Bwana Yesu, angeweza kufanya namna gani jambo hili ninalotaka kulifanya?' kisha nawe fanya hivyo; Huo ndio mwongozo wako pekee!"* Kwa maana nyingine ukitaka kuishi Injili, jaribu kufanya alivyo fanya Kristo. *"Maisha yetu yote, hata yasipokuwa na vishindo… lazima yawe yanaitangaza Injili, si katika kuhubiri kwa midomo tu bali katika mifano, na zaidi sana si kuishia kwa kuhubiri tu ila kuyaishi maagizo ya Injili.*

Kumfuasa Yesu, na ili kumpenda zaidi, inawezekana tu pale tunapomjua. Na tujamjua Yesu kwa njia ya Injili. Kwa hiyo fursa pekee kwa sisi kuwa *"Injili hai"* na kutoa miale ya upendo wa Mungu hapa duniani ni kwa kuisoma na kuisoma tena Injili mara nyingi tuwezavyo. Hii ndiyo kazi pekee iliyomwezesha Kaka Karoli alipokuwa Nazareti kuitumia kila saa aliyojaliwa kusoma Injili na kuandika mistari mirefu ya tafakari. Ili kufanya alivyofanya, tunahimizwa kuwa na muda wa kutosha kuitafakari Injili. Kwa sababu hiyo maisha ya kufanya na kushirikishana tafakari ni sehemu muhimu sana kwenye mikutano yetu.

**6.3.2 Hatua saba za kumegeana Injili: Kumegeana Biblia ni kumegeana Imani.**

(Kwa mujibu wa Askofu O. Hirmer LUMKO, Taasisi ya Afrika Kusini)

1. **Tunamwalika Mungu kati yetu**. Mmoja wetu kwa njia ya sala anamwalika Kristo kati yetu, nasi tunaifunua miyo yetu mbele ya uwepo wa Mungu.
2. **Tunasoma sehemu mojawapo ya maandiko matakatifu**. Sote tunafungua Biblia na mmoja wetu anasoma andiko lililo chaguliwa.
3. **Tunafanya tafakari. Tunaweza kuchagua neno ama aya mojawapo na kuisoma kama sala**. Najiuliza, ni neno ama aya ipi imenigusa? Kila mmoja wetu anasoma linalomgusa, anajaribu kurudia rudia ili lisikike na kupenya moyoni.
4. **Sasa ni nafasi ya Mungu kuongea tukiwa kimya**. Somo linarudiwa mara moja na tunakaa kimya kwa dakika kama tano hivi ili Mungu aseme nasi.
5. **Tunamegeana kile tulichopokea ndani ya mioyo yetu**; **tunasema kile kilichotugusa.** Hatutoi mahubiri au kufanya majadiliano. Ninawafahamisha wenzangu ujumbe nilioupokea. Tunaweza pia kushirikishana mang'amuzi ya maisha ya kiroho, mathalani mmoja wetu anaweza akatueleza amewahi maishani kuwa na mfano gani wa maisha ya kiroho kulingana na ujumbe wa leo.
6. **Tunahusisha ujumbe na wajibu uliopo kwenye kikundi**. Tuyafanye maisha yetu na kazi zetu kuongozwa na mwanga wa Neno la Mungu. Tunapata wajibu gani wa kutekeleza kulingana na neno la leo juu ya maisha binafsi na ya uhusiano katika kikundi chetu.

7. **Tunasali wote**. Kila mmoja baada ya mwingine anene kilichomfurahisha na ndani ya moyo wake anajisikiaje. Baada ya hapo tunasali na kuimba wimbo unaofahamika.

Hii ni njia mojawapo inayofaa katika kumegeana au kushirikishana ujumbe ama tafakari juu ya Injili.

6.4. **Kuabudu Sakramenti Kuu**

6.4.1. **Maana ya kuabudu.**

Kaka Karoli katika Mwongozo unaohusu maisha ya umoja anatuambia hivi: *"Tafakari ya Injili na Ibada ya kuabudu Ekaristi Takatifu ni matendo makuu ya imani yanayotuwezesha kumjua na kumpenda Yesu"*. Si rahisi kumtafakari Kristo kama hujamjua. Ili kumjua Yesu unahitaji muda wa kutosha wa kukaa naye jinsi inavyokuwa kwa wawili wapendanao wanapokuwa wameketi pamoja. Wawili hao wanaweza kukaa bega kwa bega muda mrefu hata pasipo kuzungumza chochote lakini wakawa tu wanatazamana machoni, na katika ukimya wao pendo likatawala kati yao. Kwa kweli ni jambo la ajabu, kwamba tunapokuwa kimya ndivyo nyoyo zetu zinavyojongea mbele ya ukuu wa Mungu.

Mtakatifu Theresia wa Avila katika habari ya maisha yake (tawasifu) anasema hivi: *"Ndipo sasa, naiona sala yangu ya moyo, katika akili yangu, kuwa ni uhusiano wa dhati na Mungu, najiona kuongea, ingawaje mara nyingi peke yangu, lakini naongea na Mungu anifanyaye kujisikia kuwa napendwa sana naye"*. Kuna hadithi ya mponyaji mmoja aliyewahi kumkuta mkulima akikesha mbele ya tabenakulo, na alipomwuliza kisa cha yeye kukesha pale, jibu lake lilikuwa *"Namwangalia naye ananiangalia"*.

Katika ibada ya kuabudu, tunajifunua machoni pa Mungu na kuukaribisha upendo wa Mungu upenye na kung'aa ndani mwetu. Tunapokea nguvu ya uponyaji ya Mungu na kuwa katika uangalizi wake na hivyo kujengeka katika njia zinazompendeza Mungu.

Yesu aliye katika Ekaristi ni yule yule Yesu wa Nazareti, ndiye yule yule nimsikiaye akiongea kwenye Injili. Ndiye yule yule ambaye pindo la vazi lake liliguswa na mwanamke aliyehitaji kuponywa. Kuutazama mwili wa Yesu, kutafakari juu ya Ekaristi Takatifu kwa imani, kunatuletea nguvu ile ambayo ilimtoka Kristo na ikafanya uponyaji. Kumtafakari Yesu katika maumbo ya mkate ni kumpokea Mungu kikamilifu aliye tofauti nasi lakini wakati huo huo tunajaribu kujipatanisha naye.

Kulingana na mafundisho ya Mtaguso wa Pili wa Vatikano, mageuzo ya mkate na divai si kitendo cha mazingaumbwe na chenye ukomo, bali ni kitendo kinachohusisha uwepo wa Bwana wetu Yesu Kristo na ni mwendelezo wa kazi ya kutangaza Injili, imani ya waamini, kazi za Yesu Kristo na sala za kumwomba Roho Mtakatifu. Katika sala ya Ekaristi tunamwabudu Baba kwa njia ya Yesu na pamoja naye. Na kama alivyofanya Yesu, nasi tunauombea ulimwengu. Hivyo kuabudu Ekaristi Takatifu si ibada ya mtu binafsi bali ni kitendo cha pamoja, ni mwunganiko katika Adhimisho la Ekaristi Takatifu. Ibada ya kuabudu inaitia jumuiya fundo la kuishi kikamilifu kulingana na Ekaristi. Hii si ibada tofauti na Adhimisho la Ekaristi Takatifu.

Tunaelewa ni kwa kiasi gani ibada ya kuabudu Ekaristi Takatifu ilivyokuwa na umuhimu kwa Kaka Karoli. Tutumie wasaa wa kuabudu kwa namna ile ile tunavyopenda kujizamisha kwenye maisha ya dunia ya leo. Kwa unyenyekevu tutolee sala kwa ajili ya wale wasiopenda kusali kabisa. Ibada ya kuabudu inahitajika kwetu, ili kwa njia ya subira na usikivu tuweze

kumtambua Kristo, kwa uwepo wake, matendo yake, anavyotuona katika maisha yetu ya leo, ili katika ubinadamu wetu tumuelewe alivyo (Rejea Mt. 25: 31-46).

“Ombeni, msije mkaingia majaribuni!’ (Lk 22: 40, 46; 12: 35 – 38; Mk 14: 37, 38; 13: 32-37). Hatuna budi kukesha, kuwa wastahimilivu, tunaojikumbusha kumbusha na kuwa macho ili kwamba usiwepo wakati hata mmoja ambapo tutaukatia tamaa umoja wetu na kugeukia shughuli, kazi, majukumu, mahitaji au vishawishi, ambavyo ni shinikizo linalosababishwa na hila za adui au husuda iwayo kulingana na udhaifu ama makosa yetu.

Ibada ya kuabudu inahitajika kwetu ili kuzitambua njia mbalimbali ambazo Mungu hujifunua duniani na hasa kwenye mtima wa maisha yetu. Mungu yupo duniani, lakini si wa dunia hii na haelekei kuwa hivyo. Huwezi kumtambua Mungu kama Mungu isipokuwa katika moyo wa kupenda kuabudu. “Bwana wangu na Mungu wangu”, ndivyo alivyotamka Tomaso pindi tu alipomtambua huyo aliyefufuka (Yn. 20:28).

Kaka Karoli anatutaka tushiriki ibada ya kuabudu Ekaristi kama kuwa na maongezi ya moyo na moyo na Mungu. Kaka Karoli anataka kuzichochea kwetu hisia za “Bwana” wake, hisia za Umwilisho na kudharauliwa. (Fil. 2: 7-8); anatamani tuwe na maisha ambayo ni mwendelezo wa uweko wa Ekaristi Takatifu, yaani maisha ya Ekaristi. Yesu hakuwa tu mtu, bali alijishusha hadhi. Anaunuliwa katika kipande cha mkate na anakubali kumegwa na kuliwa. Katika mkate, Yesu anajihatarisha kufanyiwa kufuru na kutoheshimiwa na kwa namna fulani anaikubali hali hii. Ndivyo Kaka Karoli anavyojitoa ili naye “aliwe’ na hatimaye ajishushe hadhi ili kila mtu aweze kumwendea. Kwa jinsi hiyo, nasi tunaalikwa kuinuliwa juu, na kutwaliwa ili kuhiyari “kuliwa”, yaani kutolea karama na wasaa wetu kwa ajili ya watu wanaotuhitaji.

#### 6.4.2 Jinsi ya kuandaa Ibada ya Kuabudu Ekaristi Takatifu.

1. Bainisha muda utakaotumika, kisha zingatia huo muda.
2. Hakikisha uko kwenye nafasi nzuri ili viungo vya mwili wako visikakamae kwa kutokuwa na sehemu nzuri ya kukaa, n.k. Unaposali, mwili wako pia unashiriki.
3. Usiruhusu mambo yatakayo kubughudhi wakati unasali.
4. Angalia kwenye Sakramenti Takatifu; litaje jina la Roho Mtakatifu na anza kwa mshukuru na kumtukuza Yesu. Namna hii itakuwezesha kujua kuwa kuna uwepo halisi wa Yesu
5. Yakabidhi mahangaiko ya ndani ya moyo wako kwa Yesu.
6. Endelea kuwa kimya kabisa (tulia, jizamishe kuabudu). Usifanye chochote hata kusali rosary au kusoma kitabu. Jiweke huru mbele za Mungu.
7. Sikiliza anachosema Bwana, Bila shaka mazungumzo yatakuwa yameanza. Jambo la muhimu ni wewe kuwa pale na kuruhusu miali ya upendo wa Mungu ikuwakie.
8. Mkabidhi Mungu yote yanayokujiri.
9. Kamilisha ama maliza kwa wimbo au sala.

### 6.5. “Kuyatazama upya maisha”.

#### 6.5.1 “Kuyatazama upya maisha” ni kufanya nini?

Kaka Karoli hakuwa ameyatazama upya maisha yake hasa kwa vile hakuishi maisha ya jumuiya zaidi ya kuishi yale ya upweke. Pamoja na hayo, bado unaweza ukaona jinsi alivyomtafuta Mungu. Daima alijibidisha kufanana na Kaka ama Bwana wake mpendwa, Yesu Kristo.

Kaka Karoli aliandika hivi *"Haidhuru kitakuwa ni kimya cha namna gani, kiwe ni cha yale maisha ya Nazareti, au maisha ya jangwani, au hata maisha ya kuonekana hadharani, lazima yawe maisha ya kuhubiri Injili kwa vitendo; maisha yetu yote, kuwako kwetu kote kutufanye tupaaze sauti ya kuhubiri Injili. Nafsi zetu zimpumue Yesu; Matendo yetu yote, maisha yetu yote sharti yalete sura ya kuwako maisha ya kiinjili. Kuishi kwetu kuwe ni mahubiri hai, ishara ya Yesu, manukato ya Yesu, yanayomfanana Yesu".*

Kwa mtazamo huu tutaweza kuishi kwa vitendo "kuyatazama maisha upya" katika Umoja wa Walei. Ili "kuyatazama upya maisha" mambo mawili ni muhimu kwa watakaoshiriki:

- Kusukumwa na nia ya kufuata Yesu wa Nazareti, nia kamili kabisa ya kutaka kubadilika, kushindana na kishawishi cha mavuno, kuweka nia ya kuwa mfuasi kamili wa Yesu, kupagaishwa naye jinsi asemavyo mtume Paulo.
- Kukubali kwa dhati kabisa ya moyo kuwa kwa njia ya Umoja Mahalia tunaweza kupata msaada na maelekezo kutoka kwa kaka na dada zetu wana umoja.

Baadhi ya mahitaji yafuatayo ni muhimu kwa ajili ya kikundi:

- "Kuangalia upya maisha" kunahitaji hali ya imani na sala katika kikundi.
- Ili "kujiangalia upya maisha" wanakikundi wawe wamezama na kufikia urafiki wa dhati na uhusiano wa karibu sana ili kila mmoja aweze kweli kuingia ndani ya maisha ya kiroho ya mwenzake.
- Kuaminiana, kuwa na busara, na heshima kuu kwa maisha ya kila mmojawapo ni vitu visivyokwepeka.
- Watakaoshiriki au watakaokuwa wakiwezesha mkutano wa "kuangalia upya maisha" lazima wazingatie kwa makini mchango wa mawazo wa kila kaka au dada anayeshiriki, kiasi cha kumwezesha atue katika kilindi cha 'kujiangalia upya' na kubaini ukweli hata kama hatafurahia.
- Ni muhimu kumwelewa kila mwanakikundi kwani umoja utajengwa si kwa kuhadithiana tu habari za maisha ya kila mmoja isipokuwa kwa kung'amua na kukidhi njia za kukuza na kudumisha umoja.

Kwa hiyo njia ya "kuyatazama maisha upya" itakuwa ni "somo la pamoja" katika maisha yetu, kwa uwezo wa mwanga wa neno la Mungu tunawezeshwa kujitazama upya. Hali hii itatufikisha kwenye uwepo wa Mungu. Aidha tunatakiwa kumbaini Yesu kwa kuishi kulingana na matakwa yake, kuishi kwa vitendo 'sala ya kujiachamanisha au kujikatalia' na hivyo kuelewa kuwa "kuyatazama upya maisha" kuna maana ya kujikatalia mengi kwa ajili ya Kristo.

"Kuyatazama maisha upya" ni nyenzo ya kukuza udugu na ushirikiano ambavyo vitatufanya kumwelekea zaidi Mungu. Hii ndiyo zawadi ya kweli kutoka kwa kaka na dada zetu kwani tunapojihusisha na ya wenzetu ndivyo Mungu anavyozidi kuwa nasi. Mungu anakuwa mtendaji kati yetu, na anafanya hivyo kila mahali na kila wakati. "Kuyatazama maisha upya" kunatuwezesha kuviondoa vikwazo vinavyotuzuia kumwona Mungu.

- Kuna vikwazo ambavyo tunaweza kuviona lakini tukawa hatuna ujasiri wa kuvikabili.
- Kuna vikwazo tunavyoweza kuvibainisha kutokana na maswali mazito wanayotuuliza kaka na dada zetu kuhusu yale tunayoshirikishana.

Jinsi walivyofanya wafuasi wa kwanza wa Yesu, ndivyo nasi tunavyoweza kuelewa Mungu anatutaka tufanye nini kwa kuangalia yaliyopita. Walichokuwa wakitafuta wafuasi wawili waliokuwa wakielekea Emmaus ndicho tunachokiita "kuyatazama upya maisha" Walipokuwa njiani "waliongea kuhusu yote yaliyotokea" (Lk 24:14). Yesu akiwa mgeni wao aliwasaidia kuyajua yaliyotukia kwa mtazamo mpya na

kuwafanya waelewe maana halisi ya matukio hayo. "*Wakasemezana: Hatukusikia moto ukiwaka ndani ya mioyo yetu pale alipokuwa akitufafanulia habari za maandiko?*" (Lk 24:32)

### 6.5.2 Mpango wa kutuwezesha "Kuyatazama maisha upya"

Kazi hii ifanyike ndani ya kikundi cha watu wachache, kwenye Umoja Mahalia wa watu wasiozidi kumi. Maandalizi yanakuwa ni kama yale ya "kuwa jangwani", sala na tafakari ya Injili daima zikiwepo.Kunahitajika mazingira ya kupenda kusikiliza, kupenda kuwa makini kwa yale anayoyatoa mwenzangu na kuyapokea, vivyo hivyo na yeye kuyapokea ninayoyatoa. Ukimya ukitawala usitutie hofu kwani yataka moyo kumdadisi mwenzako, kwa uungwana na kwa unyoofu, bila kuchelea kusababisha bughudha ama wasiwasi wowote. Moyo wa kusamehe, kuvumiliana na kuridhiana unahitajika sana katika mazingira ya kirafiki, na udugu wa kweli. Katika baadhi ya jumuiya, hutokea kwa kila mwana umoja kuandaa "mapitio" yake binafsi na kuja kuwashirikisha wenzake kwa pamoja wanapokutana.

Ufuatao ni mpango wa "Kuyatazama upya maisha" katika mfuatano wa matukio: KUONA – KUTAMBUA – KUTENDA (Rejea: Courrier Jesus Caritas Vol. XIV no. 1, August 1990, Quebec-Acadie Canada)

**KUONA**

Shabaha ya hatua hii ni kukiwezesha kikundi kumaizi mang'amuzi yake. Nini kimetendeka? Swali hili halina kusudio la kuzua mjadala bali kukifanya kikundi kimaizi, yaani kitambue kimeweza kutekeleza mambo gani katika muda uliopita. "*Nalirejesha jambo hili kwa vile nataka kuliangalia tena*". Ni kitu gani ninachokitaka?

Tutafanya vivyo hivyo!

- Kwa kufanya hivyo kila mwana umoja au jumuiya anaweza akarejea kwenye jambo lake ambalo angependa kulitazama upya ili apate mabadiliko.
- Tutarejea kwenye mambo yale ambayo tunataka tuyatazame upya kwa faida ya kubadilisha maisha yetu.

Matokeo ya kurejea kwenye mambo yaliyopita ili kuyatazama upya yana shabaha ya kutafuta na kuelewa

- Kwa nini hali imekuwa hivi?
- Jambo hili linasababishwa na nini?
- Jambo linaathiri vipi imani na mwenendo wangu?

**KUTAMBUA**

Shabaha ya hatua hii ni kuweza kujua endapo Mungu amekuwa ndiye mtendaji ama sehemu ya utendaji kwenye mambo yaliyotukia.Jambo la msingi ni kujiuliza, Ninaamini nini? Namwamini Nani?

- Nimebaini jambo gani lililo muhimu kwangu, na linanisaidiaje kukidhi matarajio yangu?
- Je jambo hili limeangaziwa na Injili na ni sehemu ya mipango aliyonayo Yesu, je nimesukumwa na hayo?
- Jambo hili linaendana na matendo gani ya Yesu kulingana na uzoefu wangu?

**KUTENDA**

Shabaha ya hatua hii ni kutuwezesha kuitika wito wa Mungu na kuujibu kwa njia madhubuti. Katika hatua hii ni lazima kuwa na uwazi, kuwa na hali ya urafiki na udugu wa kuaminiana. Baada ya kuwa nimefanya mang'amuzi kulingana na matarajio na imani niliyonayo kwa Yesu wa Nazareti:

- Nimeweza kujifunza nini?
- Napata wito wa kufanya mabadiliko gani?
- Binafsi ninaweza kutekeleza mambo yapi, Je kwa kushirikiana na wana umoja wenzangu, naweza kufanya yapi?, Na kwa kushirikiana na jumuiya nzima naweza kufanya yepi?

6.5.3 Jinsi ya "Kuyatazama maisha upya"

Washiriki wasiwe wengi au wachache sana kwani uwingi au uchache unaopita kiasi utaathiri uwezekano wa kushirikishana na hali ya kuwa wazi miongoni mwa washiriki.

- Panga muda wa kutosha.
- Andaa mazingira ya utulivu na ya kuridhisha kiasi washiriki waonje hali kama ya kuwako mafungo hivi..
- Awepo mwongozaji wa vipindi
- Anza kwa tafakari na pengine kwa sala kwa sababu "Kuyatazama maisha upya" si jambo la hivi hivi tu.
- Kumbuka kwamba kila mmoja anapaswa kuongea.
- Jali kila mtu, jali mawazo yao, na wawezeshe kujieleza kwa mbinu uwezayo na ufanye hivyo kwa taadhima.
- Ukubali ukimya ukitokea kwani ni sehemu ya maongezi yanayoendelea akilini.
- Usikate shauri kuwa mchangiaji yuko hivi au vile na uwafanye washiriki kuzingatia hilo kwani anayepata fursa ya kuongea anatushirikisha mang'amuzi kwa vile anajiamini na anawathatmini wanaomsikiliza.
- Usidiriki kutamka haya… kwamba; *"Mtu asije akafanya hivyo…", "Hata wewe unajua kwamba jambo hili ndani ya kikundi chetu halifai…", "Nimeelewa tatizo lako ni nini hasa…" n.k.*
- Mtafakari kwa pamoja ili kuona mawazo ya Bwana anayewajali wote, yanatutaka nini?
- Maelewano yanapokuwepo endelea na sala. Jaribu kuomba upatanisho wa yote.
- Kamilisha "marejeo" yaani "kuyatazama upya maisha" kwa kuruhusu mazingira ya hali ya mafungo kama awali.

**6.5.4 Muundo maanani wa "Kuyatazama maisha upya**"au namna ya kufanya "Pitio la maisha" na pia jinsi ninavyosoma Injili kutoka m'aangamuzi ya maisha yangu ni kama njia mbili ya kufanya patio la maisha:

- Kuanza na aya katika Injili na kisha kuenda katika hali halisi, au hali halisi halafu Injili.
- Kuanza na mkasa yaani yaliyotendeka na kisha kwenda kwenye Injili.

Lengo ni kuweza kuyachungulia maisha ya kila mmoja kwa mwanga wa Injili, na kujaribu kuisikia sauti ya Mungu na kuitika kwa njia ya maisha ya kila siku.

**6.6. Wasaa wa kuwa "Nazareti"**

**6.6.1 Kuwa Nazareti kuna maana gani?**

Nazareti maana yake *Mungu daima yuko nawe maishani mwako!* "Njia ya Umoja", ni dira katika safari yetu na inatujulisha habari za maisha ya kiroho ya Nazareti. Ni huko Nazareti ambako mafumbo ya

Mungu yalifunuliwa. Huko ndiko Mungu alijifunua katika sura ya kibinadamu. Na kwa ajili hiyo tunafanywa kuelewa kuwa Mungu tutamjua kwa njia ya ishara za kawaida, matukio na mambo ya kawaida yanayotuzunguka.

Daima Kaka Karoli alizama kwenye fumbo la Nazareti kwenye maisha yasiyo ya hadharani ambayo Yesu aliishi mwanzoni mwa miaka yake thelathini. Kaka Karoli alienda Nazareti kumuishi Yesu kwa ukaribu zaidi ingawaje aligundua baadaye kuwa kufanya hivyo si lazima mpaka uende Nazareti.

Cha maana si kuenda Nazareti bali ni kuwa na namna ya maisha yasiyomshinda kila mmoja yaani *"maisha ya kawaida yasiyo na makuu yanayowezakana mtu kuyaishi popote".* Utakatifu ni kwa ajili ya wote, na unawezekana katika muda wowote, katika mazingira yaliyo ya kawaida kabisa.

Nazareti ni chaguo la kudumisha upendo na kufanya kazi ya kuenjilisha kwa kujenga uelewano na ushirikiano kati ya akina baba na akina mama. Upendo na uinjilishaji utaonekana kwa njia ya sala za kawaida, kuwa na utulivu na kudumu katika kujihusisha na mambo ya kawaida ya kimaisha. Tuishi ya maisha ya kawaida lakini yenye mtizamo wa kipekee. Nazareti ina maana ya kuendelea kutakatifuza maisha yetu ya kila leo.

Nazareti ni kuishi maisha ya kidugu yenye moyo wa kujali kupeana huduma, utimilifu, kukubali ukomo katika uwezo wetu, kuwapokea wote bila ubaguzi, kumthamini kila mtu, na kuwa na mtazamo usiobeza kwa kila mtu.Uhusiano mwema humdhihirisha Mungu zaidi katika maisha yetu na hivyo unatufanya tuzidi kuimarika zaidi kama ndugu.

Nazareti ni kuwa mahali ambapo unastahili kuwa. Mahali ambapo utaweza kukuza uelewa wako kulingana na utashi wa Mungu kwako. Mahali ambapo utafanya uamuzi wa kuendelea kuhiari kujitazama upya na kutambua njia sahihi ya kutafuta maisha ya kiroho.

Nazareti ni kuishi maisha yenye matukio ya kawaida, kwani Mungu alijifanya wa kawaida kwa njia isiyo ya kawaida huko Nazareti.

### 6.6.2 Nini maana ya kuwa na "wasaa Nazareti" au kuwa na wiki "Nazareti?

Katika aya ya 4.2 kwenye "Njia ya Umoja" Nazareti inaelezwa kuwa hali ya maisha ambayo wana umoja wanatafuta ili uwezo wao uweze kuzaa matunda kulingana na hali tofauti za maisha. Kuwa na "Wasaa Nazareti" au "Wiki Nazareti" kutatutengea muda ambapo tunaimarisha mwamko na ufahamu wetu juu wito tulio nao. Tunajua kwamba mikutano ya kila mwezi haitupatii fursa tosha kukutana na watu mbalimbali, kuwa na wasaa au wiki Nazareti kutatuwezesha kushirikishana mambo ya kimaisha na wenzetu wa kada tofauti (wasio oa, wana ndoa, familia zenye watoto, vijana), kadhalika kujumuika na wale wasio wana umoja mahalia.

Wiki la Nazareti linaweza kuandaliwa kwa wana umoja katika ngazi ya taifa/nchi, ukada wenye kutumia lugha moja (kushirikisha nchi zinazopakana), kwa ajili ya bara au wanachama pacha kwa mujibu wa makubaliano. Wanachama wa matawi mengine ambayo yanashirki maisha ya kiroho ya Kaka Karoli wanaweza kualikwa. Vile vile wanachama *pweke* wanaweza kualikwa kuja kushiriki. Mikutano kama hii inaweza kutumiwa kama fursa ya kuwaalika wenye hamu ya kufahamu zidi juu ya maisha ya kiroho ya Kaka Karoli.

Shuguli katika wiki la Nazareti zaweza kuwa katika programu ya kiroho inayojumuisha mpangilia wa majukumu ya kutekeleza kila siku zikiwemo fursa za kupumzika ama burudani. Programu halisi itatokana na mazingira yaliyopo, fursa na mahitaji ya washiriki. Maisha ya kiroho ya Kaka Karoli yanapaswa kuwa chakula cha kiroho kwa wakati wote.

Vipengele vya wiki la "Nazareti" vyaweza kujumuisha

- Maisha ya pamoja
- Habari za maisha ya kiroho ya Kaka Karoli kwa kina au kwa muhtasari
- Kuyatazama maisha yetu pamoja kuona ni kwa kiasi gani tumekidhi maisha ya umoja ("Kuyatazama maisha upya", Kuabudu, Sala, kusikiliza Neno la Mungu).

Katika ratiba ya siku mambo yafuatayo yanaweza kujumuishwa:

- Sala ya Asubuhi
- Kifungua kinywa
- Neno/ majadiliano
- Kutafakari maandiko matakatifu katika vikundi
- Chakula cha Mchana
- Mapumziko au kuwa huru
- Ekaristi/Kuabudu
- Chakula cha Jioni
- Mapumziko/ muda huru
- Kuhitimisha siku pamoja katika sala ya jioni

**Mada:**

Uchaguzi wa mada awali ya yote ni jambo la muhimu. Mada iandaliwe kila siku kabla. Mada ilinge kwenye maisha kwa kuzingatia ujumbe wa Kaka Karoli. Mtoa mada anaweza kurejea kwenye maandiko matakatifu ili kuwa na jambo la kufanya tafakari na majadiliano kwenye vikundi vya watu sita sita. Mbali na kusoma na kujadiliana maandiko matakatifu, tafakari kuhusu mada ikamilishwe kwa mtu binafsi kuyatazama maisha yake na kuamua cha kufanya ili kuleta mabadiliko.

Inapofaa wakati wa asubuhi wazazi washirikiane na watoto wao kuona shughuli wanazoweza kufanya huku wakioanisha yale yaliyowasilishwa kwa njia ya mada ya siku iliyotangulia. Zinaweza kuandaliwa programu rasmi kwa ajili ya watoto. Nyakati za mchana washiriki wana uhuru wa kushiriki shughuli za pamoja kujitenga; mtu anaweza kuchagua kushiriki ibada ya kuadhimisha Ekaristi au kwenda kuabudu Ekaristi Takatifu.

Kutahitajika siku kamili au la nusu siku pindi itakapokuwepo siku ya "jangwani" kumwezesha mtu kufanya tafakari, ambayo matokeo yake anaweza kuwashirikisha washiriki wote kwenye nyakati za Ekaristi ama wakati wa majadiliano kwenye vikundi. Fursa kama hii ya kuwa "jangwani" ni wakati pekee, hivyo yafanyike maandalizi ili mahitaji yakila mmoja yaweze kupata la kukidhi.

Pale inapowezekana, sakramenti kuu inaweza kuwekwa mahali ambapo mtu anaweza kwenda wakati wowote kuabudu wakati wa wiki ya "Nazareti". Kwa namna hii washiriki wanaweza wakajitenga na wenzao wakati wowote wa sala ilimradi kupata wasaa wa kuabudu kulingana na mahitaji ya mtu binafsi na hivyo kuzikabidhi tafakari mikononi mwa Mungu.

**6.7 Siku ya kuwa "Jangwani".**

**1. Umuhimu wa mang'amuzi ya kuwa "jangwani" katika mchakato wa kukomaa kiroho.**

Tukilitaja jangwa, mawazo yetu yanapata picha ya eneo halisi kijiografia la mahali jangwa lilipo- ambako mchanga umetanda na mitende iliyo ota ota sehemu zenye chemichemi inakuwako. Hata hivyo jangwa lina uzuri wake. Kaka Karoli aliishi katika mazingira haya ya jangwa miongoni mwa Watuareg. Sisi tulio wengi hatujapata bahati kama hii, lakini tunaweza kupata picha kama hiyo ndani ya mioyo yetu.

Katika mtizamo wa kibiblia, jangwa ni hatua kuelekea lengo mojawapo. Huendi jangwani kuishi bali ni mahali pa kuvuka ama kupita. Sote tunaikumbuka habari ya Kutoka ambapo kwa miaka 40 hivi "Taifa teule" lilipitia jangwani kuelekea nchi ya ahadi. Waisraeli walitembea kutoka utumwani hadi kuwa huru. Safari yao ilifanyikia jangwani. Kwa kukabiliana na majaribu na mateso mengi Waisraeli waliweza kujifunza jinsi ya kuenenda na Mungu wao. Mungu aliwaongoza, aliwalinda, aliwalisha, aliwanywesha na alikaa nao hadi walipoingia nchi ya ahadi. Kadhalika katika Injili tunasoma jinsi Yesu alivyoonja maisha ya kuwa "jangwani". Kwa kuenda jangwani Yesu aliweza kujiandaa kwa kazi yake ya ukombozi. Alikabiliana na vishawishi vya kupata mamlaka, ufahari na anasa. (Mk 1,12-13).

Kwao Waisraeli na kwa Yesu. "jangwa" lilikuwa ni:

- Mahali pa kukutana na Mungu
- Mahali pa kujinyenyekeza
- Mahali pa kupata vishawishi
- Mahali pa maasi
- Mahali pa kuomboleza
- Mahali pa ukimya
- Mahali pa sala
- Mahali pa hazina iliyofichika
- Mahali pa ukamilifu
- Mahali pa kujitazama upya
- Mahali pa neema.

"Jangwa" laweza kutustahilia hayo yote endapo tutalipokea katika maisha yetu. Tulitafutie nafasi"jangwa" ndani ya maisha yetu. Tujitengenezee "jangwa" ili tuwe watulivu.

Tukiwa wanachama wa Umoja wa Walei wa Kaka Karoli tunahimizwa kuwa na walau siku moja ya kuwa "jangwani" kadiri ya utaratibu tutakaojiwekea. Tunahitaji kuwa mbali na kelele za aina mbalimbali ili tupate kuirejea Biblia. Hali hiyo itarejesha nyoyo zetu kutoka mawazo mengine na hivyo kujitanabahi (kujitambua) wenyewe na kumtanabahi Mungu. Wema na huruma ya Mungu ndivyo vinavyotuongoza "jangwani" ambako tunaenda kwa ajili ya kusali. "Jangwani" ni wasaa unaofanya tujitambue tulivyo dhaifu, maskini na watu wadogo sana, tuliogubikwa (tuliojawa) kiburi na uovu, uvivu na ubabaikaji.

Mang'amuzi hayo ni muhimu kwa ajili ya kukua kwetu kiroho. Tunaing'amua njaa na kiu yetu na kujikuta tunangojea wema na huruma ya Mungu. ("Ukweli utawaweka huru". Yn 8: 32). Mchakato wa kukomaa kwetu kiimani unapatikana "jangwani".

Hata hivyo "jangwa" si mwisho wa yote; ni hatua moja kwenye safari na ni hatua muhimu. Kama wanadamu tunahitaji kuwa na nyakati za ukimya, kujitenga na kutoonekana. Tunapokuwa "jangwani" tunapata nguvu na kuimarika katika kuwajali kaka na dada zetu wahitaji na hivyo kuwakaribisha wote nyoyoni mwetu.

### 6.7.2 Siku ya kuwa “jangwani” inavyokuwa

Panga siku iwayo na andika kwenye shajara ili uizingatie. Kumbuka siku ya kuwa “jangwani” si kwenda mapumziko!

**1. Maandalizi:**

- Chagua utakakokwenda “jangwani”, mathalani kijijini, kanisani, chumbani mwako, n.k.
- Ni muda gani muafaka kwenda? Naweza kutenga muda kiasi gani? Asubuhi tu au mchana? Tenga muda maalum wa sala.
- Nitakuwa “jangwani” peke yangu au nahitaji kuwa na mtu mwingine. Panga vizuri kabla.
- Nitahitaji nini? Chakula kidogo… daftari za kuandikia… Biblia…. Mwavuli…
- Jambo gani litakuwa mada kuu katika kutafakari kwangu? Hatua muhimu ninazozihitaji kuzichukua kimaisha… kujiandaa kufanya uamuzi fulani… kujihisisha na utatuzi wa mgogoro binafsi, wa kifamilia, wa wanandugu, n.k… somo la kuchagua mfano Injili… “Nayatazama maisha upya”)

**2. Siku yenyewe ya kuwa “jangwani”**

- Epuka mazingira ya usumbufu
- Anza mapema iwezekanayo, kumbuka muda uliopo ni azizi (mali)
- Siku ya kuwa “jangwani” haimanishi kujificha au kuzagaa tu. Itafaa kujipa mazoezi kwa kutembea umbali utakao kuwezesha kijisikia vizuri. Jaribu kujipa amani kwa undani.
- Upe mwili wako usikivu kwa kujali haja zake, hasa mahitaji ya kawaida.
- Jaribu kufanya vitu vya kawaida kama kujipumzisha, kutulia, kutabasamu, kuwaza waza, kujihusisha na jambo mojawapo, n.k.
- Tafuta maswali mazito na yachimbue kwa undani hata usipokubaliana nayo.
- Jihadhari na kukosa raha lakini usijiachie hilo likakusumbua.
- Fanya tafakari kuhusu somo la Injili, sala au dhamira yoyote.
- Tafakari maisha yako mbele ya Mungu
- Shabaha ya kuwa na siku ya “jangwani” ni kujitafiti ili uweze kujihusisha na wenzako tena.
- Zingatia ratiba ya kusali uliyojipangia, jitenge ili upate muda wa kuwa na Mungu.
- Fanya tathimini mwisho wa siku (Nimeona nini kilicho kizuri au kibaya. Kuna ninachoweza kukifanya). Ingefaa uandike yale unayoyakusudia kuyatekeleza.
- Urudipo nyumbani elewa kuwa wito wako uko hapo na kuwa hauko “jangwani”
- Inawezekana ungependa kumshirikisha mtu mang’amuzi yako hasa rafiki, mkeo, mumeo, padri, mshauri). Inapobidi, jaribu kupanga naye.

### 6.8 Kimarisha Maisha ujumbe wa kiroho wa Kaka Karoli.

Kuna mbinu mbalimbali zakutuwezesha kuingia katika undani wa ujumbe wa kiroho wa Kaka Karoli. Bado tunahitaji undani kuhusu maisha yake, jinsi alivyoongoka, safari yake ya kiroho, chaguo lake la maskini, uamuzi wake wa kuishi kwa unyenyekevu maisha ya “Nazareti”.

Mojawapo ya mbinu zilizopo ni pamoja na

- Kusoma vitabu (angalia orodha), kitabu kimojawapo kinaitwa “Pamoja na Karoli wa Foucauld katika kuishi Injili”,
- Machapisho kama vile Umoja wa Walei kitaifa na kimataifa, Familia ya kiroho ya Karoli wa Foucauld;

- Mikutano ya matawi ya familia ya kiroho,
- Kanda za video,
- Wavuti,
- Mafungo,
- Matukio maalum: Maadhimisho ya Desemba Mosi, Wakati wa kuwa "Nazareti", mikutano ya wanaumoja mahalia, n.k.

### 6.9. Ahadi kwenye Umoja wa Walei

Namna wazi ya kuweka ahadi inahitajika katika Umoja wa Walei ili kuthibitisha kuwa mmojawapo ameamua kwa dhati kuwa mmojawapo wa Wana Umoja wa Walei.

Kwa atakayehitaji kuwa mwana Umoja wa Walei lazima atimize yafuatayo:

- Akubaliwe na wana umoja mahalia
- Abainishe anatarajia kitu gani kwake binafsi na kutoka kwenye umoja.
- Afanye "Kuyatazama upya maisha" mara kwa mara ili uamuzi atakaoufikia uwe kweli ni uamuzi huru na wa kina.
- Endapo anayeomba kujiunga atahitaji kufanya tendo la nje yaani jambo inaloonekana ili kudhihirisha ahadi anayoweka, tukio linaweza kutayarishwa lakini si jambo linalopaswa kuwa la lazima sana.

### 6.10 Kushiriki majukumu

Kadiri inavyowezekana, kukutana kwa pamoja kufanyike kwa zamu nyumba hadi nyumba. Na kila kunapofanyikia mkutano, waendeshaji wawe ni wenyeji wenye nyumba.

### 6.11 Kushiriki kwenye majukumu ya huduma za umoja

*"Kwenye Umoja ndiko mahali wajibu unakotekelezwa kwa pamoja… Huduma za uratibu, huwa mikononi mwa wachache, hata hivyo kwa wachache kukabidhiwa jukumu la kuratibu majukumu haiwi kikwazo kwa wengine kushiriki katika utendaji wa pamoja."* (Sheria Namba 30, Ufaransa)

*"Mawasiliano kati ya vikundi mbalimbali ndani ya umoja ni jambo muhimu kwani huwa ni ushuhuda hai wa umoja; maisha ya mmoja huwa chakula kwa wanaumoja wote. Ni hazina inayofaa wote waipate kwa viwango viwavyo: kikundi, jimbo, nchi, dunia".* (Sheria Namba 32, Ufaransa)

Kila umoja mahalia uchague atakayehusika kuwa kiungo na wana umoja wengine (katika mji, jimbo, kanda, nchi, dunia) kulingana na muundo wa umoja katika nchi husika. Katika ngazi zote wajibu huu utengewe muda rasmi, yaani utendaji uwe ni katika muda utakaotajwa.

# SURA YA 7
# SALA

**“Sala ya kujiachilia” ya Kaka Karoli**

**Utangulizi**

Sala hii ni matokeo ya tafakari za Kaka Karoli juu ya injili, tafakari ambazo zimekusanywa hapa na pale. Tafakari zake zililenga hasa juu ya ‘fadhila kuu’ na aliandika tafakari hizi mnamo 1896 akiwa Siria. Wakati huo alikuwa angali akijulikana kwa jina lake la utawa wa ndani la Kaka Maria Alberiki. Kama kuna anayeistahili kusali sala hii basi ni Yesu pekee, kwa sababu tukiisali sisi inatuwia mno. Endapo tunaisali kama sehemu ya familia yake ya kiroho basi

a) Ni kwa sababu twajua ya kuwa si sisi tunaoisali peke yetu, isipokuwa Yesu ndiye kwa njia yetu anaisali.
b) Ni kwa sababu tunawezeshwa na Yesu katika nia yetu ya kujiachisha ili tuweze kuunganika naye aliyekabidhi kujiachisha kwake kwa Baba yake.

Sala hii inatualika kuunganika na Yesu. Inalenga kuyaelekeza maisha yetu kwa Mungu na kwenye ule ubinadamu ambao Yesu alitutangulia. Inatutia moyo kujiachisha kwa ujasiri mbele ya Baba.

**Historia ya “sala ya kujiachisha”**

*Mawazo yafuatayo yanatokana Na makala ya Antoni Chatelard, Kaka Mdogo wa Yesu, ambaye amechambua sala hii pengine kuliko yeyote aliyewahi kuwa mwana Familia ya Kiroho.*

Sala kwa mara ya kwanza ilitumika wakati wa kutangaza kifo cha kaka mdogo wa kwanza (Marc Gerin) huko Abiodh, Aljeria. Sala ya kujiachisha pia ilichapishwa kwa mara ya kwanza kwenye jarida la Umoja wa Kaka Karoli wa Foucauld.

Tangazo hilo la kifo lilipokuwa likitolewa ndipo aya mojawapo ya barua ya mwanafunzi mwenzake na Marc Gerin iliyokuwa imeandikwa hiyo sala ilinukuliwa. Bila shaka Marc alikuwa amewasambazia rafiki zake sala hiyo. Yeye Marc yawezekana aliipokea sala hiyo kutoka kwa Dada mdogo Magdalena wa Yesu wakati alipomtembelea hospitalini 1945.

Dada wadogo walikuwa tayari wakiisali sala hiyo kila siku kwa muda upatao miaka minne hata kabla ya novisiati ya kwanza 1940. Mnovisi mmojawapo Dada mdogo. Marguerite wa Yesu anatujulisha:

*“Nakumbuka vizuri sana siku ambapo Dada mdogo. Magdalena alivyotualika mimi pamoja na dada mdogo Anna kusoma tafakari ya Kaka Karoli, sehemu inapopatikana sala hii.*

*Jioni hiyo aliniambia: ‘Huoni kwamba hii ni sala nzuri sana, kwa nini tusiitumie kama sala yetu kila siku?’ Tulikubaliana na kuona vema tukiisali kwa sauti. Tulihitaji kuondoa sehemu zilizojirudia rudia, na ndivyo tulivyofanya pamoja na kazi ya kuihariri. Sala inayotumika sasa ndiyo hiyo tuliyoiikamilisha jioni ile. Nyongeza tuliyoipachika ni ya neno ‘leo’. “Utende nami leo utakavyo”. Baada ya hapo tumekuwa tukisali kila asubuhi hadi siku ambapo kaka wadogo walipotusihi tuisali nyakati za jioni,, na ndipo tukalitoa neno “leo”.*

Hatimaye neno tulililoliongeza la ‘leo’ likawa limetoweka hadi kufikia 1944, jinsi anavyoshuhudia katika shajara yake dada mdogo Magdalena (25/08/1942) ambapo sala hii imeandikwa kikamilifu. Kuelekea 1955, ikawa imekuwa mazoea kuisali sala hii nyakati za jioni, baada ya tafakari fupi ya siku.

**7.1.2 "Sala ya kujiachisha"**

**Baba,**
**Najitia kabisa katika mikono yako,Unitendee lolote utakalo**
**Na lolote utakalonitendea nitakushukuru.**
**Niko tayari kupokea kila kitu,Ikiwa mapenzi yako yatatimizwa ndani yangu,**
**Na katika viumbe vyako vyote.**
**Sitamani mengine kuliko haya.**
**Ninaiweka roho yangu mikononi mwako,**
**Ninaitoa kwako kwa upendo wa moyo wangu wote,**
**Kwa kuwa ninakupenda ee Bwana**
**Na ndiyo maana ninahitaji kujitoa kwako pasipo kiasi,**
**nikiwa na matumaini yasiyo na mwisho**
**Kwa kuwa u Baba yangu,Amina.**

## Veni Creator – Uje Roho Mtakatifu

### 7.2.1 Utangulizi

Kaka Karoli aliandika 'mashauri ya kiinjili' katika kipindi kati ya Pasaka na Pentekoste 1908, kwa ajili ya mapadre, watawa waume kwa wake, kwa wana ndoa na wasio na ndoa, ili waweze kuiyaishi maisha ya Nazareti, hadi waishi kikamilifu kulingana na maisha hayo. Vile vile kama msaada wa kuweza kuishi Injili katika maisha yao ya kila siku. Ibara ya XI ya 'mashauri ya kiinjili' inahusu sala. Kaka na dada wanaalikwa kusali mara tatu kwa siku; Asubuhi, Adhuhuri na Jioni. Veni Creator ikiwa sala mojawapo. Aliandika:
*Veni Creator, ikisaliwa katika nyakati tatu kuu za siku, yawa maombi ya kaka na dada walioko uhamishoni kwa Baba yao wa Mbinguni, ili kumwomba amtume Roho wake Mtakatifu, 'mkate wa kila siku' na 'kile kilicho stahili yetu' kwa ubinadamu wetu ambacho amekiumba, kwa kila saa atupatiayo huku 'bondeni kwenye machozi'. Kaka na Dada waweke nia yao yote kwenye kusali sala hii, wakiwaombea wote- wake kwa waume bila ubaguzi"*
Katika maandishi aliyoyatumia nyakati za mafungo sala hii imeonekana mara nyingi kwake Kaka Karoli, na katika barua ya Septemba 19, 1911 aliyomwandikia Louis Massignon, ni kumbukumbu zinatotufanya tuamini kuwa aliisali sala hii mara kwa mara.

1. Veni, Creator Spiritus, mentes quorum visita: imple superna gratia, quae tu cresti pecora

2. Que diceris Paraclitus, donum Dei altissimi, fons vivus, ignis, caritas fons vivus, ignis, caritas et spiritalis inctio.

3. Tu septiformis munere, dextrae Die tu digitus, tu rite promisum Patris sermone ditans guttural.

4. Accende lumen sensibus, infunde amorem cordibus, infirma nostril corpis virtute firmans perpeti.

5. Hostem repellas longius pacemque dones protinus; ductore sic te previo omne noxium.

6. Per te sciamus da Patrem noscamus atque Filium, te utriusque Spiritum credamus omni tempore.

1. Njoo Roho Mtakatifu,
Angalia zetu nyoyo,
Waletee neema nguvu,
Wakosefu viumbevyo.

2. Majina yako: Mfariji,
Shina la uzima, pendo
Wake Mwenyezi upaji,
Mafuta ya roho, moto.

3. Ndiwe mnye mapaji saba
Wa Mungu kuume mkono,
Mshika uhadi wa Baba,
mtoa kwa ndimi maneno.

4. Angalo litung'arie,
Moyo kwa pendo tushtushe,
Nguvu, neema, tujalie,

Wanyonge wathibitishe.

5. Mbali shetani mkimbize,
Na amani tupatie;
Tukufuate, tuongoze,
Na maovu tukingie.

6. Baba Mungu tujulishe,
Pia mwana tumkubali,
Roho, tuunganishe,
Mtokea wao wawili.

7. Atukuzwe Mungu Baba,
Na wake Mwana Mfufuka,
Naye Roho Mtakatifu na milele yote Amina

Sasa K. -Peleka Roho wako nao wataumbwa
W. -Na uso wa nchi utafanywa upya

**Tuombe:** Ee Mungu uliyezifundisha nyoyo za waamini wako ukiwaletea mwanga wa Roho wako Mtakatifu, twakuomba utujalie kwa njia ya huyo Roho tuweze kuyajua yaliyo mema na tujazwe faraja zake , kwa njia ya Kristo Bwana wetu, Amina.

**Uje Roho Mtakatifu (Tafsiri rahisi)**

1. Uje, Roho Muumbaji,
Mtoaji wa uzima,
Watuimarisha imani,
Wadumisha matumaini yetu.

2. Uje, Roho wa Upendo,
Wawaunganisha wakristo kimapendo,
Wawaonesha kuishi kwa amani,
Kila mtu wamfanya mtumishi wa wote.

3. Uje Roho mmwenye huruma,
Watupatanisha sisi, Waleta maelewano
kati yetu,
na waondoa ugumu wote.

4. Uje paji la nguvu,
watutia imara kukabili,
Watufanya kupenda kweli,
na Watupeleka kwa Mungu.

5. Uje Roho wa Mwanga,
Tujulishe kwa Baba,
Tujulishe kumjua Mwana,
Tuwezeshe daima kukuamini,
Wewe uliye kiunganishi
cha Baba na Mwana,
Kwa pendo la pekee. Amina.

Tulibariki jina la Bwana
Tumshukuru Mungu.

)

6. Uje, Roho Muumbaji,
   Mtoaji wa uzima,
   Watuimarisha imani,
   Wadumisha matumaini yetu.

7. Uje, Roho wa Upendo,
   Wawaunganisha wakristo
   kimapendo,
   Wawaonesha kuishi kwa amani,
   Kila mtu wamfanya mtumishi wa wote.

8. Uje Roho mmwenye huruma,
   Watupatanisha sisi, Waleta maelewano
   kati yetu,
   na waondoa ugumu wote.

9. Uje paji la nguvu,
   watutia imara kukabili,
   Watufanya kupenda kweli,
   na Watupeleka kwa Mungu.

10. Uje Roho wa Mwanga,
    Tujulishe kwa Baba,
    Tujulishe kumjua Mwana,
    Tuwezeshe daima kukuamini,
    Wewe uliye kiunganishi
    cha Baba na Mwana,
    Kwa pendo la pekee. Amina.

    Tulibariki jina la Bwana
    Tumshukuru Mungu.

**Sala ya "Malaika wa Bwana"**

Sala ya Malaika wa Bwana ni hazina iliyojawa mafundisho ya imani na moyo wa kuabudu kulingana na mapokeo ya Kanisa Katoliki kwa ajili ya kumheshimu Maria Mama wa Yesu. Kwa kusali tunakumbuka fumbo la Umwilisho kila tunapoitikia baada ya Kusali Salamu Maria mara tatu na halafu sala maalum ya kuhitimisha. Kawaida "Malaika wa Bwana" husaliwa Asubuhi, Adhuhuri na Jioni. Alipokuwa Nazareti Kaka Karoli alitafakari mara kwa mara juu ya kupashwa habari Maria kwamba atamzaa Yesu na Maria kumtembelea Elizabeti. Kaka Karoli alijisikia kana kwamba anamleta Yesu katika ulimwengu ulioshindwa kumtambua. Kaka Karoli anaonelea ni vema tuisali sala hii ili tuweze kumkubalia Mungu jinsi Maria alivyofanya huko Nazareti.

### 7.3.2 Malaika wa Bwana

Malaika wa Bwana alimpasha habari Maria: Naye akapata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu

Salamu Maria umejaa neema, Bwana yu pamoja nawe, umebarikiwa kuliko wanawake wote na Yesu mzao wa tumbo lako amebarikiwa, Maria Mtakatifu Mama wa Mungu utuombee sisi wakosefu sasa na saa ya kufa kwetu. Amina.

Ndimi Mtumishi wa Bwana: Nitendewe ulivyonena.

Salamu Maria…

Neno akatwaa mwili: Naye akakaa kwetu.

Salamu Maria….

Utuombee mzazi Mtakatifu wa Mungu: Tujaliwe ahadi za Kristo.

Tuombe: Tunakuomba Ee Bwana utie neema yako mioyoni mwetu, ili sisi tuliojua kwa maelezo ya malaika kwamba mwanao amejifanya mtu kwa mateso na msalaba wake tufikishwe kwenye utukufu wa ufufuko. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu Amina.

# SURA YA 8

# HABARI MBALIMBALI

**8.1 Mawasiliano kwa njia ya mtandao**:

Wavuti ya kimataifa: www.charlesdefoucauld.org kuna taarifa mbalimbali zikiwemo

- Taarifa na kumbukumbu za vitabu na matini juu ya Kaka Karoli wa Foucauld na maisha yake ya kiroho, katika lugha mbalimbali.
- Anwani za matawi ya Familia za Kiroho za Kaka Karoli
- Matukio na habari za hivi karibuni.

Wavuti zaidi za kimataifa:
www.jc.gn.apc.org
www.brothercharlesofjesus.org
n.k, n.k.

**8.2. Chapisho Rasmi la kimataifa**

Chapisho rasmi la kimataifa hutolewa mara mbili kwa mwaka katika lugha za kifaransa, kiingereza na kihispania. Baadhi ya habari hutafsiriwa kwenye lugha za kiarabu na kikorea. Ili kupata nakala ya Chapisho hili, wasiliana na wana timu ya Kimataifa.

**8.3. Ishi Injili pamoja na Kaka Karoli wa Foucauld.**

Chapisho hili ni kwa ajili ya wanaohitaji kujua zaidi maisha ya kiroho ya Kaka Karoli, na vilevile kwa ajili yao ambao ni wana umoja lakini wanataka kujiimarisha kiroho na kujitoa zaidi kwa njia ya kusoma, kufanya tafakari, na majadiliano. Kunapatikana rejea muhimu kutoka kwenye biblia

na kutoka kwenye maandiko ya Kaka Karoli pamoja na maswali kwa ajili ya “kuyatazama maisha upya”. Ili kuweza kupata “Kuishi Injili” wasiliana na wana timu ya kimataifa.

**8.4 Karoli wa Foucauld na familia yake ya kiroho**

Hiki ni kijarida chenye matawi 19 ya familia ya kiroho ya Kaka Karoli, kikiwa na maelezo kuhusu kila familia, idadi ya wanachama na sifa za kila tawi (njia ya maisha, utume, vipengele muhimu). Vile vile kunapatikana anwani za mahali wanafamilia mbalimbali wanapopatikana duniani. Ili kupata nakala wasiliana na wanatimu ya kimataifa.

**Ili kupata nakala zaidi wasiliana na wana timu ya kimataifa au walei wana umoja.**

Kempen, Ujerumani: 2006.

Tafsiri imefanywa na:
Baltazari Sungi
SLP 487
SINGIDA
bmukhortya@yahoo.com